epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumamosi Januari 18, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
ISSN 0856 • Na. 0581925
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
MWANGA WA JAMII

## MKUTANO MKUU CCM


# Macho, masikio yote ni Dodoma

• **Kiu** mrithi wa Kinana yaongezeka, wajasiriamali wafurahia fursa... *Endelea Uk.3*




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan akiongoza Kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), jijini Dodoma jana. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Visiwani na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na kulia ni Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 22
**NEYMAR: MBAPPÉ ALIMWONEA WIVU MESSI**



UKURASA WA 2
**Saratani** ya utumbo mpana sasa tishio jipya



UKURASA WA 4
**Mtoto** miaka miwili adaiwa kuibwa mbele ya wazazi wake

UKURASA WA 5
**TCRA** yaonya wasiozingatia masharti ya utangazaji

## Mawakili wa Dk. Slaa wazua tafrani kortini
UKURASA 2

Aliyekuwa Balozi, Dk. Wilbroad Slaa, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza wakati akitolewa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kuelekea mahabusu baada ya kukosa dhamana kutokana na shtaka linalomkabili la kuchapisha taarifa za uongo katika mitandao. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



## Mume wa DC Mahawe asimulia maneno aliyosema mkewe kabla ya kufariki dunia
UKURASA 15

**MICHEZO** **YANGA GUSA, ACHIA TWENDE ROBO FAINALI** UK.24 **KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, ASP Emmanuel Kandola (kulia), akizungumza na madereva wa mabasi ya shule wakati wa zoezi la ukaguzi wa magari hayo, wilayani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mawakili wa Dk. Slaa wazusha tafrani kortini

**Na Grace Gurisha**

JOPO la mawakili wa mwanasiasa mkongwe nchini, Dk. Wilibrod Slaa, likiongozwa na Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Boniface Mwambukusi, limemwashia moto Hakimu Mkazi Mkuu Beda Nyaki wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, baada ya kutokusikiliza maombi ya kupinga dhamana ya mteja wao.

Moto huo ulianzishwa jana na Wakili Hekima Mwasipu ndani ya chumba cha wazi namba mbili cha mahakama hiyo, baada ya Hakimu Nyaki kukubaliana na jopo la mawakili wa serikali kwamba wasubiri kwanza uamuzi wa pingamizi la uhalali wa hati ya mashtaka ndipo maombi ya kupinga dhamana yasikilizwe.

Baada ya tu hakimu kukubali kwamba kesi inaahirishwa hadi Januari 23, 2025 kwa ajili ya uamuzi huo, Wakili Mwasipu alisimama na kuzungumza kwa sauti ya juu kwa kutuhumu kwamba kinachoendelea si haki kwa mteja wao.

Wakili Mwasipu aliwageukia mawakili wa serikali na kuwaeleza kwamba wanachokifanya si haki kwa kuwa Dk. Slaa ni mzee ana miaka 76 ni mgonjwa pia ni kama mzazi wao.

"Hebu mwangalieni huyu mzee ni kama mzazi wenu. Anaweza kuwazaa nyie, hivyo mnachokifanya si haki. Tulishakubaliana sasa hivi mnakataa, si haki hata kidogo huyu mzee ni mgonjwa nyie," alidai Mwasipu.

Sauti ya Mwasipu ilimsimamisha kwa hasira na jazba Mwambukusi ambaye alipiga vitabu vyake juu ya meza huku akidai kwamba si haki kwa sababu tayari walishakubaliana kusikiliza pingamizi pamoja na maombi hayo, hivyo kwa nini hakimu abadilike.

Chumba cha mahakama kiliendelea na mrindimo wa kelele, huku mmoja wa jopo la mawakili hao akimtaka Hakimu Nyaki kama hawezi kusikiliza kesi hiyo ajitoe kuliko kufanya anachokifanya.

Wakati hayo yote yanaendelea, Hakimu Nyaki alikuwa kimya akiwaangalia tu kwa sababu ni hali ambayo ilisababisha taharuki na asijue nini cha kufanya kwa kile ambacho kimetokea mbele yake kutoka kwa mawakili wa Dk. Slaa.

Kutokana na ukweli kwamba tayari Hakimu Nyaki alikuwa ameshapanga tarehe ya usikilizwaji kwa kesi hiyo, alitoka katika chumba hicho bila kutoa mashambulizi yoyote wala kujibu.

Kelele hizo ziliendelea huku wakidai kwamba hawaondoki mahakamani hapo bila Dk. Slaa. Hata hivyo, askari Magereza waliokuwa ndani ya chumba hicho, takribani sita, walimwondoa Dk. Slaa haraka na kumpeleka moja kwa moja ndani ya basi la Magereza na kuondoka.

Baada ya hapo, mawakili walidai kwamba wanakwenda kufungua shauri la maombi ya mapitio Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kutokana na kutoridhishwa na uendeshaji wa kesi hiyo unavyoendelea.

Wakati hayo yote yanaendelea, Dk. Slaa alikuwa akitabasamu tu na alipoulizwa na ndugu yake mmoja mbona haonekani kushtuka, alisema hayo ni mambo ya kawaida katika masuala ya siasa, Dk. Slaa amerudisha rumande.

Mbali na Mwambukusi na Mwasipu, mawakili wengine wanaomtetea Dk. Slaa ni Edson Kilatu, Peter Madeleka, Sanga Melikiole, Sisty Aloyce na Mwanaisha Mndeme.

Jopo la mawakili wa serikali linaongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Tawabu Issa, Clemence Kato, Michael Ngoboko, Nura Manja wakisaidiana na mawakili wa Serikali Abdon Bundala na John, lilikuwa kimya likiangalia kinachoendelea wakati mawakili wa Dk. Slaa wakizusha tafrani hiyo .

Hakimu Nyaki alisema ni vyema maombi ya dhamana yakasikilizwa baada ya uamuzi wa kupinga uhalali ya hati ya mashtaka kutolewa.

Awali, wakiwasilisha pingamizi juu ya hati hiyo ya mashtaka, Madeleka alidai kuwa anawasilisha pingamizi lao chini ya Kifungu 131 A (1)(4) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) Sura ya 20 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2021.

"Kwa mujibu wa rekodi za mahakama kesi hii imeletwa mara mbili tofauti huku upelelezi ukiwa haujakamilika na sheria iko wazi kwamba ni marufuku kuleta kesi ya jinai ambayo haipo serious mahakamani kama upelelezi haujakamilika," alidai Madeleka.

Alidai kuwa katika kifungu hicho kimetaja kesi ambazo zinatakiwa kuletwa kwa mahakamani bila upelelezi kukamilika, shtaka analoshtakiwa nalo mteja wao lipo chini ya sheria ya mtandao.

"Kwa mtu yeyote aliyesoma sheria vizuri na kuhitimu na mwenye akili timamu hawezi kushindwa kuelewa kwamba mashtaka ya mtandao sio mashtaka serious yaliyotajwa kwenye sheria hii."

"Kwa hiyo kwa kuwa wenzetu wasomi na nguli wa sheria wamethibitisha upelelezi haujakamilika wala hawajakiona hicho kifungu wanaomba tarehe nyingine ya kutajwa sisi tunaona hicho kinatosha kuiondoa kesi hii."

Alidai kuwa kesi ya namna hiyo inapopelekwa mahakamani upelelezi unatakiwa uwe umekamilika, kwa maana hiyo Mahakama ni sheria iliundwa kwa Katiba kwa mujibu wa kutenda haki." Ni takwa la lazima la Katiba yetu kesi ifuatwe mteja wetu aachiwe huru kwa sababu limeletwa kinyume cha sheria."

Akijibu hoja hizo, Wakili Issa alidai kuwa katika tafsiri ya kawaida katika hicho kifungu lipo shtaka ambalo linaendana na la kuchapisha taarifa ya uongo, tafsiri yake ni kuweka wazi taarifa ambazo zinahatarisha usalama wa umma, ni miongoni mwa mashtaka ambayo hayana dhamana.

Dk. Slaa anatuhumiwa kusambaza taarifa za uongo kupitia mtandao wa X ( Twitter), ilidaiwa kuwa kosa hilo alilitenda Januari 9, mwaka huu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mtandao huo wa kijamii, kupitia jukwaa lililosajiliwa kwa jina la Maria Salungi Tsehai @MariaSTsehai kwa lengo la kupotosha umma.

***Kwa maoni: +255 677 020 701. Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Kansa ya utumbo mpana sasa tishio jipya

**Na Restuta James**

TAARIFA 'mbaya' kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) ni kwamba ulaji wa nyama nyekundu, vyakula vya kusindika, vyenye mafuta mengi bila matunda na mboga, umeongeza wagonjwa wa saratani ya utumbo mpana.

Saratani hii imeongezeka nchini, ikitajwa kuwaathiri vijana kuanzia miaka 40. Hata hivyo, saratani ya kizazi na matiti, bado inaongoza.

Akizungumza na Nipashe Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa ORCI, Dk. Julius Mwaiselage, alisema kwa wastani hospitali hiyo inapokea wagonjwa watatu wa saratani ya utumbo mpana kila siku.

Dk. Mwaiselage anasema miaka 10 iliyopita, aina hiyo ya saratani haikuwa inatajwa nchini, lakini hivi sasa ipo kwenye orodha ya aina 10 tishio. Anasema kuna ongezeko la aina hiyo ya saratani duniani.

"Tanzania imeongezeka sana na inatokea katika umri mdogo. Zamani ilikuwa inatokea katika umri mkubwa, lakini miaka ya karibuni inatokea kwa watu wenye umri mdogo.

"Chanzo cha kwanza ni kama kuna historia kwenye familia, cha pili ni mtindo wa maisha hasa ulaji usiofaa kama matumizi ya nyama nyekundu, vyakula vilivyosindikwa, vyenye mafuta (unene), kutokula matunda na mboga mboga.

"Tofauti na ilivyokuwa hapo awali, ilikuwa inatokea kwa watu wenye miaka 60 na kuendelea, Tanzania inatokea wastani wa miaka 40. Umri wa katikati wa kufanya kazi," anasema.

Kwa mujibu wa Dk. Mwaiselage, takwimu zinaonesha kwamba wastani wa umri wa watu kupata saratani nchini ni miaka 45 hadi 50, wengi wakiwa wanawake wanaopata kwenye mlango wa kizazi na matiti.

Anasema mbali ya ongezeko la wagonjwa wa saratani ya utumbo mpana, saratani zinazoongoza nchini na asilimia kwenye mabano ni ya shingo ya kizazi (35), matiti (15), njia ya chakula (10), ngozi (TISA), muunganiko wa saratani ya kichwani, mdomoni na shingoni (nane), tezi dume (saba) na utumbo mpana (sita).

Hali hiyo, anasema inatokea pia kwenye nchi zilizoendelea kama Marekani na Ulaya, ambako raia wa nchi hizo walikuwa wanapata saratani wakiwa na umri mkubwa kuanzia miaka 60 hadi 90 na kwamba kwa sasa wagonjwa wanabainika hata katika umri wa miaka 50.

Anasema kwa nchi kama Marekani wanapata saratani katika umri mdogo kwa sababu ya kuongezeka kwa visababishi vya saratani na jitihada za kugundua ugonjwa huo mapema. Taarifa hiyo ya Dk. Mwaiselage inakuja siku chache baada ya Jumuiya ya Saratani ya Marekani, kubaini kwamba vijana wa kike wako hatarini kupata saratani.

"Saratani ya matiti huchangia karibu nusu ya uchunguzi wote wa saratani kwa wanawake walio na umri wa chini ya miaka 50," alisema Rebecca Siegel, mwandishi mkuu wa utafiti huo na mkurugenzi mkuu wa kisayansi wa utafiti wa jumuiya hiyo.

HABARI KITAIFA

MKUTANO MKUU MAALUM CCM



Sehemu ya Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi CCM Taifa (NEC), wakiwa kwenye kikao jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Macho, masikio ya Watanzania Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MACHO na masikio ya Watanzania Dodoma. Ndivyo ilivyo kutokana na Mkutano Mkuu Maalum wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuanza leo jijini hapa ambao pamoja na mambo mengine, wajumbe takriban 2,000 watamchagua Makamu Mwenyekiti wa CCM, Bara kwa kupiga kura ya Ndiyo au Hapana.

Nafasi hiyo inajazwa baada ya aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo, Kanali (mstaafu) Abdulrahman Kinana, kuomba kupumzika mwishoni mwa Julai, mwaka jana.

Mbali na kumpata Makamu Mwenyekiti Bara, Mkutano Mkuu Maalum unatarajia kupokea taarifa za utekelezaji wa kazi za serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kwa kipindi cha mwaka 2022 hadi 2024.

Hata hivyo, kiu kubwa ya wanachama, wapenzi, wakereketwa na wafuasi na wapenzi wa siasa kwa ujumla, ni kujua nani atachukua nafasi hiyo nyeti ndani ya CCM.

Nafasi hiyo, mbali na anayeshika kuwa msaidizi wa Mwenyekiti upande wa Tanzania Bara, pia ina uzito wa kipekee uliowekwa na kanuni za Maadili na Uongozi za CCM, zinazomtambua kuwa ndiye Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya Udhibiti ya Kamati ya Usalama na Maadili Taifa ndani ya chama hicho.

Kamati hiyo, inaundwa na wajumbe wanne, ikiongozwa na Makamu Mwenyekiti Bara kama Mwenyekiti wengine ni Mkurugenzi wa Maadili ngazi ya taifa kama Katibu na wajumbe wawili wa Kamati Kuu kutoka Zanzibar na Bara.

Kamati hiyo ndiyo yenye wajibu wa kusikiliza, kuhoji na kupendekeza adhabu kwa watuhumiwa wenye mashtaka yanayopelekwa kwa uamuzi, kwenye vikao vya ngazi ya juu. Wakati wa uchaguzi mkuu, kamati hiyo ndiyo ambayo huchambua na kupendekeza wanachama wanaowania nafasi mbalimbali katika uwakilishi wa dola, zikiwamo za ubunge na wa-tia nia ya urais.

Kwa mantiki hiyo, nafasi hii inahitaji kumpata mtu imara atakayesimamia masuala ya kimaadili hasa kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu na suala la wanachama kuzingatia maadili ni jambo la msingi. Ulegevu wowote katika nafasi hiyo unaweza kusababisha chama kupata wagombea wasio na maadili wala sifa za uongozi.

Pia Makamu Mwenyekiti anayetakiwa kwa wakati huu ni yule ambaye atakuja kufanya kazi ya kuivusha salama CCM katika Uchaguzi Mkuu wa 2025.

### WARITHI WATARAJIWA

Hadi sasa kuna watu kadhaa wanatajwa na kuzungumzwa kuwa huenda wana sifa za kushika nafasi hiyo kurithi 'viatu' vya Kinana.

Makada wanaotajwa kuwa huenda watashika nafasi hiyo ni Waziri Mkuu Mstaafu na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya CCM, Mizengo Pinda, Abdallah Bulembo, Stephen Wasira.

Kutokana na hekaheka za mkutano huo, Nipashe jana ilitembelea katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma na kuona barabara za kuingia katikati ya jiji na kuelekea ukumbi wa mkutano huo wa Jakaya Kikwete zikiwa zimepambwa kwa bendera na mabango yanayosomeka 'Karibuni Mkutano Mkuu Maalum wa CCM Taifa', mengine yakionesha kazi zilizotekelezwa chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuandikwa 'Ametekeleza'.

Pamoja na kupambwa kwa mabango hayo, upatikanaji wa vyumba katika hoteli pamoja na nyumba za kulala wageni umekuwa wa shida tofauti na wiki moja iliyopita.

### WAJASIRIAMALI WAFUNGUKA

Mmoja wa wajasiriamali anayeuza sare za CCM, Trabo Bwenda, alisema ametokea mkoani Morogoro kwa ajili ya kuchangamkia fursa za mkutano huo kwa kuwa wajumbe wanahitaji kuwa na sare ili kushiriki vikao na mkutano huo.

Mfanyabiashara wa kuku katika Soko la Miembeni, Hussein Ali, alisema kufanyika kwa mkutano huo kumeongeza mzunguko mkubwa wa biashara kutokana na kuongezeka mahitaji ya kuku choma.

"Unajua wageni wanapokuja Dodoma hasa kwa wingi wakati huu wa mkutano wa CCM wengi wao wanajua Dodoma wanapatikana kuku wa kienyeji, hivyo kunakuwa na uhitaji mkubwa wa kuku wa kuchoma. Tumejiandaa kuhakikisha kwa kipindi chote wanapatikana ili kukidhi mahitaji hayo," alisema.

Naye mamalishe Mwadawa Omary alisema wameanza kuona ongezeko la wateja wa chakula kuanzia jana kutokana na wingi wa watu ambao wamewasili kwa ajili ya mkutano huo.

"Ninaamini kwa siku hizi tatu ambazo vitafanyika vikao vya CCM tutapata kipato kikubwa hata wenzangu wanaochoma kuku, nyama na kuuza vinywaji tunatarajia tutanufaika na mkutano huu," alisema.

> Ninaamini kwa siku hizi tatu ambazo vitafanyika vikao vya CCM tutapata kipato kikubwa hata wenzangu wanaochoma kuku, nyama na kuuza vinywaji tunatarajia tutanufaika na mkutano huu.

Mtendaji wa Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Dodoma, Ringo Ilingo, alisema fursa anazoziona kwenye mkutano huo ni kwa wawekezaji wa vyumba vya kulala wageni, watoa huduma za vyakula watanufaika na mkutano huo.

Alisema halmashauri za mkoa wa Dodoma zinatakiwa kutumia fursa hiyo kuonesha maeneo ya uwekezaji ikiwamo wa hoteli zenye hadhi ya kimataifa na nyumba za kulala wageni zenye ubora.

"Maeneo mengi ya kulala wageni bado hayana ubora kwani hoteli nyingi bado ni nyumba za chini taasisi za fedha zinatakiwa kutoa mikopo kwa watu kuwekeza maeneo ya huduma hizi za malazi. Hivi sasa Dodoma inakwenda kuwa mji wa kitalii, hivyo lazima kuanza kujipanga," alisema Ringo.

Pia alisema kwa sasa Dodoma kuna mahitaji makubwa ya nyama lakini uzalishaji upo chini hivyo kushauri kuwapo na wawekezaji wa machinjio za kisasa ili kuongeza uzalishaji.

Juzi, Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makala, alizungumza kwenye moja ya vyombo vya habari kuwa wageni na wajumbe 3,500 wanatarajia kuhudhuria mkutano huo.

Mkutano huo mkuu, jana ulitanguliwa na vikao vya Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) vikiongozwa na Mwenyekiti Rais Samia Suluhu Hassan. Vikao hivyo pamoja na kuandaa Mkutano Mkuu Maalum, pia vilitarajiwa kupendekeza jina la atakayechukua nafasi ya Kinana.

# Mtoto adaiwa kuibwa mbele ya wazazi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro linamsaka mwananchi anayedaiwa kumwiba mtoto Shamimu Ndihagule, mwenye umri wa miaka miwili.

Mtu huyo anadaiwa kumwiba mtoto huyo kutoka kwa wazazi wake wanaoishi katika kitongoji cha Kisiwani, Kijiji chaTunda, Kata ya Kidodi Wilaya ya Kilosa mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Alex Mkama, alithibitisha jana kuibwa kwa mtoto huyo majira ya asubuhi Januari 15, mwaka huu, kutoka kwa wazazi wake wanaoishi katika kitongoji hicho.

Alisema mtoto huyo alichukuliwa na mtu asiyefahamika wakati anacheza na mtoto mwenzake aitwaye Josephat Jangama, mwenye umri wa miaka mitatu, ambaye mkazi wa kitongoji hicho.

Kwa mujibu wa Kamanda Mkama, wakati watoto hao wanacheza, alitokea mtu asiyejulikana na kumchukua Shamimu na kutokomea naye katika mashamba ya miwa.

"Baada ya taarifa hiyo, tumeanza msako mkali na unaendelea wa kumtafuta mtoto huyo, hivyo tunaomba mwananchi yeyote mwenye taarifa zitakazosaidia kupatikana kwa mtoto huyo aziwasilishe kituo chochote cha polisi au ofisi yoyote itakayosaidia kupatikana kwa mtoto huyo," alisema Mkama.

Katika hatua nyingine, Rashid Mussa (24) ambaye ni mwenye ulemavu wa ngozi na mkazi wa kitongoji cha Kimbawala kijiji cha Kiziwa, Kata ya Kiroka wilayani Morogoro, amefariki dunia baada ya kuanguka kutoka juu ya mnazi.

Kamanda Mkama alithibitisha kutokea kwa tukio hilo akibainisha kuwa awali Janauri 13, mwaka huu, kwenye kituo cha Polisi Morogoro ilitolewa taarifa ya kutoweka kwa kijana huyo.

Mkama alisema taarifa hiyo ilisema kijana huyo alitoweka katika makazi ya mzazi wake, Juma Mussa Juma (45), mkulima na mkazi wa kitongoji hicho na haikujulikana amekwenda wapi.

Alisema baada ya kupokea taarifa hiyo , polisi ilifanya ufuatiliaji wa kina na ilipofika Januari 15, mwaka huu, majira ya alasiri, katika kitongoji hicho kijana huyo alipatikana akiwa amefariki dunia nchini ya mnazi mrefu na pembeni yake kulikuwa na nazi 14 ambazo zilianguliwa kutoka kwenye mnazi huo.

Mkama alisema uchunguzi unaonesha kuwa Rashid alianguka kutoka juu ya mnazi hadi chini na kufa papo hapo wakati akiangua nazi kwenye mashamba ya nazi.

# Mfuko nishati safi kunufaisha wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI inaendelea na ukamilishaji wa taratibu za kuanzisha Mfuko wa Nishati Safi ya Kupikia ili kuweka ruzuku itakayowawezesha wananchi wa kipato cha chini kumudu bei ya gesi.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, aliiarifu Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira jana jijini Dodoma, alipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya mwaka ya shughuli za kamati iliyowasilishwa bungeni Februari, mwaka jana.

Alisema kanuni za usimamizi wa miradi ya biashara ya kaboni zimebainisha ruzuku kupitia hakimiliki za kaboni zinazopatikana kutokana na kupunguza matumizi ya nishati inayochafua mazingira, hivyo ruzuku hiyo ni sehemu ya juhudi za kitaifa za kutekeleza malengo ya kupunguza gharama kwa watumiaji wa nishati safi.

Khamis aliieleza kamati hiyo kuwa katika jitihada za kupunguza gharama za matumizi ya nishati mbadala, serikali imetia saini makubaliano ya awali na wawekezaji kuhusu ruzuku ya Sh. bilioni 8.64 kwenye nishati safi ya kupikia na majiko 452,455 yamepata ruzuku.

Aidha, Naibu Waziri alisema serikali inaendelea kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala kwa njia mbalimbali ikiwamo utoaji wa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari na ziara za viongozi.

Pia alisema Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kushirikiana na wadau wengine wakiwamo Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuhamasisha na kuhimiza halmashauri zote za vijiji kuainisha misitu yote ya vijiji yenye sifa ya kuingizwa kwenye mpango wa biashara ya kaboni.

Alisema uhamasishaji wa jamii kuhusu umuhimu wa biashara ya kaboni katika kuhifadhi mazingira na kuongeza kipato kwa jamii unaendelea kutolewa kwa wananchi.

Pia alisema serikali inaendelea kusimamia na kuhakikisha mikataba ya biashara ya kaboni inanufaisha wananchi na inafanyika kwa mujibu wa kanuni za usimamizi wa biashara ya kaboni.



Mfanyabiashara mdogo maarufu machinga, akibeba mabegi kutafuta wateja katika eneo la Posta, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wajasiriamali waitwa kwenye Wiki ya Sheria

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kahama, imewaita wajasiriamali kujitokeza na kuonesha bidhaa zao katika viwanja vya mahakama Wiki ya Sheria ili kukuza biashara zao.

Kadhalika, wametakiwa kufika ili kupata elimu mbalimbali ikiwamo kuandika wosia na mirathi itakayokuwa inatolewa na mahakimu na mawakili.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Edmund Kente, aliyabainisha hayo juzi wakati akizungumza kwenye kikao na wadau wa mahakama ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya maadhimisho ya Wiki ya Sheria inayotarajia kuanza Januari 25 mpaka Februari 3, mwaka huu.

Alisema wajasiriamali wana wajibu wa kutumia viwanja vya mahakama katika kuonesha na kutangaza bidhaa ili wapate wateja na kukuza biashara zao katika kipindi hicho.

Kante alisema hatua hiyo itasaidia pia timu ya mahakama kuwafikia kwa haraka na kuwapatia elimu ya masuala mbalimbali ya kimahakama kuliko kumfuata mmoja mmoja katika shughuli zao. Alisema wale walioko vijijini au pembezoni watumie viwanja vya mahakama za mwanzo katika kuonyesha bidhaa zao na kuwataka mahakimu wa mahakama hizo kutumia fursa hiyo katika kuwaelimisha wananchi ili washiriki kikamilifu shughuli za mahakama pamoja na kuwaondoa hofu pale wanapohitajika kutoa ushahidi.

Pia alisema Wiki ya Sheria mwaka uliopita, waliweka mikakati ya kupambana na mawakili vishoka ambao walikuwa wakiwalaghai wananchi, kuwachukulia fedha na kuwapotezea muda na walifanikiwa.

Alisema mkakati huo ulifanikiwa kutokana na wananchi kupewa elimu ya namna ya kuwapata mawakili kupitia E-Wakili na wale ambao walikuwa na shaka nao waliwaripoti na kuchukuliwa hatua. Aliwataka wazazi na walezi kutimiza wajibu wao wa malezi kwa vijana wao kwani kuna mashauri mengine yanafika mbele ya mahakama yanahitaji tu malezi na itasaidia kuondoa msongamano wa mahabusu.

# ZEC kuandikisha wapigakura wapya 79,000

**Na Suleiman Rashid Omar,**

PEMBA

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), inatarajia kuandikisha wapigakura wapya 78,922 waliotimiza umri wa miaka 18 kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 katika uandikishaji wa awamu ya pili kwa mwaka huu.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji George Kazi, alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa wadau wa uandikishaji wa wapigakura wapya awamu ya pili kwa mwaka 2025 katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Wete-Pemba.

Alibainisha kuwa uandikishaji huo utaanza katika wilaya ya Micheweni Februari Mosi, mwaka huu, na kumalizika katika wilaya ya Mjini Machi 17, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Jaji Kazi, uandikishaji huo ni matayarisho ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 pia ni uandikishaji wa mwisho kuelekea katika uchaguzi huo.

Kuhusu lengo la kufanya mkutano huo, alisema Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina utaratibu wa kukutana na wadau kila linapotokea jambo muhimu ambalo linahitaji kuwashirikisha.

Sambamba na hilo, alisema Tume kupitia mikutano hiyo inasikiliza maoni, hoja na mapendekezo yatakoyosaidia kuendesha uandikishaji huo kwa ufanisi.

Alisisitiza kwamba uandikishaji huo utawahusu wapigakura wapya ambao hawajaandikishwa katika Daftari la Wapigakura na utafanyika kwa muda wa siku tatu kwa kila wilaya kwa mujibu wa ratiba iliyotangazwa na tume.

Mwenyekiti huyo aliwaomba wananchi waliotimiza sifa kujitokeza kutumia haki yao ili kushiriki katika uchaguzi wa mwaka 2025 na kuwakumbusha kwamba huduma za uendelezaji wa Daftari zinaendelea katika ofisi za ZEC wilaya muda na saa za kazi.

Aliwaomba wananchi na wadau wote wa uchaguzi Zanzibar kudumisha amani katika kipindi chote cha uandikishaji wa wapigakura wapya kama walivyofanikisha katika kisiwa cha Pemba na matumaini yake kwamba wataendelea kushirikiana katika mustakabali mwema wa uchaguzi wa taifa.

Akiwasilisha taarifa na utaratibu wa uandikishaji wa wapigakura wapya na uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Thabit Idarous Faina, alisema ZEC inatarajia kuweka wazi orodha ya wapigakura waliopoteza sifa na wanaohamisha taarifa zao kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 19 na 31 cha Sheria ya Uchaguzi na 4 ya mwaka 2018 wakati wa uwekaji wazi wa orodha ya wapigakura walioandikishwa katika uandishaji wa awamu ya pili.

Alisema ZEC inaendelea kutoa huduma ya ujumbe mfupi wa simu ya mkononi ambapo wapigakura wanaweza kujua taarifa zao kwa kutumia simu ya mkononi kwa mitandao yote iliyosajiliwa Tanzania na huduma hii ni bure na haina makato.

Pia aliwaomba wananchi na wadau wote wa uchaguzi kwa ngazi tofauti kushirikiana na Tume kufikisha ujumbe huu kwa wananchi ili kuwahamasisha wananchi wenye sifa za kujiandikisha kufika vituoni wakiwa na kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi.

"Kila mwananchi anawajibu wa kwenda kituoni kuangalia jina lake ama

kuona jina la mtu ambaye hahusiki kuwamo kwenye daftari hilo ama kwa kufariki dunia au kwa namna nyingine yoyote," alisema.

Naye Maulid Ame Mohammed, Mkurugenzi wa Huduma za Sheria akiwasilisha mada ya nafasi ya Sheria katika Uandikishwaji na Uendelezaji wa Daftari la Wapigakura, alisema kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kila Mzanzibari aliyetimiza miaka 18, ana haki ya kujiandikisha na kupiga kura katika uchaguzi unaofanyika Zanzibar.

Akifunga mkutano huo wa wadau, Kamishna wa Tume hiyo, Awadh Ali Said, aliwataka wadau kutambua majukumu yao pamoja na kuwa wakweli katika changamoto zinazojitokeza wakati wa uandikishaji ili kazi hiyo ifanyike kwa ufanisi bila uvunjifu wa amani.

Juma Kombo Hijja (Sibure) ambaye ni Mratibu wa Umoja wa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar (UWZ) alivishauri vyama vya siasa kuwahamasisha wapigakura kwa kauli za kistaarabu na si kutoa kauli ambazo zinaviashiria vya uvunjifu wa amani.

Alisema viashiria hivyo vitasababisha kundi la watu wenye ulemavu kutojitokeza katika uandikishaji wapigakura wapya.

Mkutano huo umeshirikisha wadau mbalimbali wa uchaguzi ikiwamo taasisi za serikali na binafsi, vyama vya siasa, makundi maalum, vyombo vya ulinzi na usalama na vyombo vya habari.



Mamalishe wakiendelea na shughuli zao kando ya barabara, eneo la Mikocheni Viwandani, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana, mazingira ambayo ni hatarishi kiafya kutokana na kukosa huduma muhimu kama maji na vyoo. **PICHA: JOHN BADI**

# TCRA yaonya wasiozingatia masharti utangazaji

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imeonya watoa huduma za utangazaji wanaokiuka vipengele kadhaa vya kanuni za utoaji maudhui kuwa itaendelea kuwachukulia hatua stahiki za kiudhibiti na kiusimamizi.

Taarifa ya hali ya mawasiliano Tanzania iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, jijini Dar es Salaam jana, inaonesha maeneo ya ukiukwaji yaliyothibitishwa baada ya ufuatiliaji wa maudhui ya televisheni 16 na redio 12 zenye leseni za kitaifa kati ya Oktoba na Desemba, mwaka jana.

"Maeneo ambayo watoa huduma wengi wa televisheni wamekiuka ni kwenye uzingatiaji wa ratiba ya vipindi, dakika zinazotakiwa kwa taarifa ya habari," alisema.

Alisema utaratibu wa TCRA wa maombi ya leseni za maudhui ya redio na televisheni unawataka waombaji kueleza jinsi watakavyohakikisha ubora wa vipindi, faida za vipindi kwa uchumi wa jamii. Pia wanatakiwa kuwasilisha ratiba ya vipindi kabla ya kuanza kuvitoa na kuizingatia. Ratiba inatakiwa kueleza muda, mpangilio na idadi ya vipindi.

Taarifa hiyo ya TCRA inaonesha kuwa televisheni sita kati ya 16 zilizotathminiwa zilizingatia ratiba iliyowasilishwa Mamlaka mapema. Hii ni pamoja na kuwa 12 kati ya hizo ziliwasilisha ratiba.

Watoa huduma wamefanya vizuri kwenye utoaji wa maudhui ya ndani, ambapo kanuni zinataka yawe angalau asilimia 60 na kwenye vipindi vya elimu.

Hata hivyo, matokeo ya ufuatiliaji huu yanaonesha mabadiliko kulinganisha na Septemba 20254 ambako redio zote 12 zilizopitiwa zilikiuka masharti ya kuzingatia ratiba.

Huduma za televisheni zinatolewa kupitia mitambo iliyosimikwa ardhini (DTT), kwa njia ya madishi ya setelaiti (DTH) na kwa waya. Mifumo ya DTT na DTH inahitaji visimbuzi ambavyo vinapokea maudhui na kuyawezesha kuonekana kwenye televisheni.

Takwimu zinaonesha kuwa Desemba 2024 kulikuwa na visimbuzi 2,148,763 vilivyolipiwa vifurushi.

Kampuni tano zina leseni za kutoa huduma za kusambaza maudhui kupitia ving'amuzi. Hizo na idadi ya visimbuzi vya mfumo wake kwenye mabano ni Azam TV(1,340,135), Star Media (477,527), Multichoice Tanzania (225,263), Agape Associates (1,840), Basic Transmission - Digitek (15,000), Continental (67,663) na Wananchi Cable (21,335).

Azam Media Limited ina idadi kubwa ya visimbuzi vya DTT vilivyolipiwa vifurushi ikilinganishwa na watoa huduma wengine, ikifuatiwa na Star Media Limited. Kwa ujumla, idadi ya visimbuzi vya DTH vilivyolipiwa vifurushi ni vingi kuliko visimbuzi vya DTT.

Idadi ya televisheni zinazopokea maudhui kwa njia ya waya iliongezeka kutoka 15,781 Machi 2024 hadi16,767 Desemba 2024. Shinyanga inaongoza kwa kuwa na 4,219, ikifuatiwa na Mwanza (2,070) na Tabora (1,872).

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga wasiingie uwanjani na matokeo yao

**LEO** Yanga ina kibarua kigumu na muhimu cha kusaka pointi tatu muhimu za kuwapeleka hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa namna msimamo wa kundi A wa michuano hiyo, Yanga ina kila sababu ya kupata ushindi ili kufuzu kwa mara ya pili mfululizo hatua hiyo ya robo fainali.

Yanga ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo ikiwa na pointi saba chini ya wapinzani wao wa leo MC Alger wenye pointi nane huku Al Hilal wakiongoza kundi wakiwa na pointi 10, hizo zote ni kabla ya michezo ya leo.

Kutokana na hilo, MC Alger nao wamejipanga na wamejiandaa kikamilifu kwa ajili ya mchezo wa leo kwani wanafahamu umuhimu wa ushindi kwa kuweza kutinga robo fainali.

Hata hivyo kimahesabu ni kama Waarabu hao wana machaguo mawili kwenye matokeo ya leo, sare yoyote kwao ina faida na watakuwa wamefuzu moja kwa moja kucheza robo fainali.

Ugumu wa mchezo wa leo unawafanya Yanga kutoingia uwanjani wakiwa na matokeo yao kichwani, wanapaswa kuingia kwa tahadhari na kupambana kwa muda wote kuweza kupata ushindi utakaowapeleka robo fainali.

Wachezaji wafahamu mashabiki wao wapo nyuma yao, kitu pekee cha kufanya ni kuhakikisha wanapambana muda wote ndani ya uwanja na kucheza kwa tahadhari kubwa kwa sababu hawana chaguo lingine zaidi ya ushindi tu.

Matokeo zaidi ya ushindi yatawafanya msimu huu kuishia hatua ya makundi kitu ambacho si malengo yao na hata mashabiki wao watahuzunika sana hasa baada ya kuona wapinzani na watani zao wa jadi, Simba wakitinga robo fainali ya michuano Kombe la Shirikisho Afrika.

Utamaduni wa soka letu, Simba na Yanga ni watani ambao kila mmoja anaombea mwenzake asifanikiwe ili wapate nafasi ya kuchekana na kutaniana na kunogesha soka letu.

Mpaka sasa katika Kombe la Shirikisho Afrika, Simba yenyewe tayari imeshajihakikishia kucheza robo fainali, kesho itaingia uwanjani kucheza na CS Costantine kusaka nafasi ya kuongoza kundi lao.

Yanga wamepoteza nafasi ya kuongoza kundi lao, lakini bado wana nafasi ya kufuzu robo fainali kama tu watafanikiwa kupata ushindi kwenye mchezo wa leo dhidi ya wapinzani wao MC Alger.

Yanga wana nafasi ya kufikia hatua hiyo, lakini lazima wajipange uwanjani, wacheze kwa nidhamu kubwa, wawanyime nafasi wapinzani wao kumiliki mpira.

Tunataka kuikumbusha Yanga tabia za Waarabu katika hatua kama hizi wanapowania nafasi ya kusonga mbele hasa wanapokuwa ugenini, kama watafanikiwa kupata goli la kuongoza watacheza mpira wa kupoteza muda.

Lakini watataka kucheza zaidi na mwamuzi kwa maana ya kulalamika sana, watacheza mpira wa taratibu na kupoteza muda sana kwa kujiangushaangusha.

Ili kuyaepuka haya yote, Yanga wanapaswa kuchanga karata zao vizuri kwa kuhakikisha wanaanza wao kupata bao na kuhimiri kasi yao Waarabu wanapotafuta bao, hakuna kinachoshindikana.

Nipashe tunazitakia kila la heri klabu zetu zote, Yanga kutinga robo fainali na Simba kupata ushindi utakaowafanya kuingia robo fainali wakiwa wanaongoza kundi lao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kufungiwa Simba iwe fundisho

**WAKATI** mwingine kwenye maisha si lazima kulipiza kisasi. Na mara nyingi anayelipiza kisasi huonekana kuwa ndiye mwenye matatizo. Unaweza ukaonewa au kufanyiwa kibaya watu wasione, lakini ukiamua kurudisha au kulipiza kisasi kila mmoja atakushukia kuwa umetenda ndivyo sivyo.

Hata wale waliopo magerezani kwa sasa wamefungwa, baadhi yao wamefanya hivyo kwa kulipiza kisasi. Kwa maana hiyo tunajifunza kuwa makini sana na kitu cha kurudishia, au kulipa kisasi.

Hiki ndicho kilichowakuta mashabiki wa Simba. Baada ya kuchokozwa kidogo tu na mashabiki wachache wa CS Sfaxien, wakaamua kuwarudishia. Kibaya zaidi ni kwamba wao walikuwa wengi dhidi ya mashabiki wachache wakorofi ambao hawakuwa na uwezo wa kujitetea kwa chochote pale walipofanyiwa vurugu.

Nasema Simba ilifanyiwa vurugu nikirejea taarifa rasmi ya Jeshi la Polisi iliyotolewa, Desemba 15 mwaka jana baada ya kumalizika kwa mchezo huo.

Taarifa hiyo iliyotolewa na Kamanda Kanda Maalum ya Polisi, (SACP) Jumanne Muliro, ilibainisha kuwa kulitokea fujo kwenye mchezo huo uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa baada ya kumalizika kwa mchezo kati ya Simba dhidi ya CS Sfaxien.

"Fujo hizo zilisababishwa na mashabiki wa timu ya CS Sfaxien kutoridhika na maamuzi ya refa wa mchezo huo kuchezesha mechi kwa dakika zaidi ya saba ambazo zliziongezwa kama dakika za kufidia zile zilizopotea jambo ambalo lilisababisha Simba kupata bao la pili na la ushindi.

Wachezaji ndani ya uwanja na benchi la ufundi la timu hiyo walikasirika, wakaamua kumfuata mwamuzi wa mchezo na kuanza kufanya vitendo vya kumshambulia.

Katika fujo hizo, shabiki mmoja wa CS Sfaxien aliumia na kupatiwa huduma ya kwanza, akaruhusiwa, huku viti vya rangi ya bluu 156 viking'olewa na mashabiki pamoja na vya rangi ya mchungwa 100," ilisema sehemu ya taarifa hiyo ya Polisi.

Hii ni taarifa iliyojitosheleza kabisa kwani imeainisha kila kitu mpaka sababu.

> **Ni nadra sana kuona timu za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Kusini na hata Magharibi zikifungiwa. Mara nyingi timu zinazopewa adhabu hizi ni za Afrika Kaskazini.**

Kwa maana hiyo baada ya kuchokozwa mashabiki wa Simba walishindwa kuzuia hasira zao, badala yake sasa wamefungiwa kuingia uwanjani katika mechi ya kesho dhidi ya CS Constantine.

Awali mashabiki wa Simba walipanga kujazana uwanjani kwani kwao si mechi ambayo ilikuwa ya presha sana kwa sababu tayari wameshatinga robo fainali.

Kwao ilionekana ni ya kwenda 'kuinjoi' zaidi, kwa sasa hali sivyo ilivyo tena. Watalazimika kubaki majumbani, kwenye vipanda umiza na wengine wameambiwa waende Temeke Mwembeyanga ambako kutafungwa TV kubwa.

Ni nadra sana kuona timu za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Kusini na hata Magharibi zikifungiwa. Mara nyingi timu zinazopewa adhabu hizi ni za Afrika Kaskazini.

Timu karibuni zote kubwa za Afrika Kaskazini zimeshakutana na kadhia hii, wenyewe ni kama wamezoea na ndiyo sehemu ya maisha yao, lakini siyo huku.

Mashabiki wa Simba wameonekana kuhuzunika na adhabu hii, hili lisiwe fundisho kwa mashabiki si wa Simba tu, bali wa timu zote za Tanzania ambazo timu zao zitafuzu kucheza michezo ya kimataifa msimu ujao.

Mashabiki wajifunze 'fair play' na uvumilivu wakiwa uwanjani, na kuepuka kukubali kuchokozeka kirahisi na wapinzani hasa mashabiki wa Afrika Kaskazini ambao wao kufanya fujo na kufungiwa ni kama sehemu tu ya utamaduni.

Mfano, sikuona sababu ya mashabiki wa Simba kuwa na hasira kiasi kile kwani tayari timu yao ilikuwa imepata bao la pili, badala yake wangekuwa wanashangilia zaidi kuliko kupigana na wageni wao.

Nadhani baada ya hili kutokea, mashabiki wote Bongo watakuwa wamejifunza na hawatorudia tena kwani CAF hawangalii mtu usoni, wala kuionea aibu klabu kwa sababu ni kubwa au ndogo, kwani sheria na kanuni ni kama msumeno, unakata huku na huku.

# Maofisa elimu waonywa rushwa uhamisho wanafunzi

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma imewaonya maofisa elimu kata, jiji na wadhibiti ubora wa elimu watakaobainika kuomba rushwa kwa wazazi au walezi ili kuwasaidia uhamisho wa wanafunzi.

Pia TAKUKURU imewaonya walimu wanaouza vipindi vyao vya darasani kwa walimu wengine ili kwenda kuendelea na majukumu binafsi na kwamba watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria kwa sababu hiyo ni rushwa pia.

Ofisa Uchunguzi Kiongozi Msaidizi TAKUKURU Dodoma, Faustine Malecha, alisema hayo jana wakati akitoa elimu kwa maofisa elimu ngazi ya kata, jiji na maofisa udhibiti ubora wa elimu katika mkutano uliolenga kuangalia mitaala mipya ya elimu iliotolewa na serikali.

Malecha alisema kumekuwa na minong'ono mingi mitaani juu ya baadhi ya maofisa hao kuwaomba wazazi fedha ili kuwasaidia kuhamisha watoto shule.

Alisema kutokana na kuwapo kwa madai hayo, TAKUKURU imeanza kulifanyia kazi suala hilo ili kuhakikisha kama lipo linatokomezwa katika maeneo mbalimbali.

"Hakuna sababu ya kuomba rushwa kwa wazazi ili umsaidie kumpa uhamisho wa mwanafunzi. Hilo ni kosa unachopaswa kufanya ni kutekeleza jukumu ulilopewa wakati unaingia kazini," alisema Malecha.

Pia alisema hakuna sababu ya maofisa kufanya vitendo hivyo na kama wanavifanya wanapaswa kuviacha kwa sababu TAKUKURU haitawaacha salama pale baadhi yao watakaobainika na makosa hayo.

Naye Idda Siriwa, Mwelimishaji Umma kutoka TAKUKURU Dodoma, aliwataka maofisa hao kuwa makini na vitendo vya rushwa kwa sababu vinachangia kuharibu na kurudisha nyuma maendeleo ya taifa.

Alisema jamii hususani kundi hilo la maofisa elimu kuanzia ngazi ya kata, jiji pamoja na maofisa udhibiti ubora wa elimu mkoani hapa, wanapaswa kuwa mstari wa mbele kukemea vitendo vya rushwa na si kuvikumbatia.

"Tunaomba zingatieni hii elimu ya kuzuia rushwa itawasaidia kulinda heshima na utu wenu kwenye utumishi wa Umma, mkifanya hivyo hamtakumbana na rungu ya rushwa," alisema Siriwa.

Alisema utoaji elimu unaofanywa na taasisi hiyo ni wa kuzingatia kwa sababu wasipofanya hivyo itawawia vigumu kujua madhara yatokanayo na mtu kupokea rushwa kutoka maeneo mbalimbali.

Mashaka Manjalloh, Ofisa Udhibiti Ubora wa Shule Jiji la Dodoma, aliishukuru TAKUKURU kutokana na kuwakumbusha wajibu wao pale wanapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Alisema elimu waliopewa ni ya muhimu kwa sababu tatizo la rushwa limekuwa changamoto kwa baadhi ya watu hususani pale wanapohitajika kutoa msaada kwa jamii ili kufanikisha kile wanachokiomba kutoka kwenye

# Serikali kuendelea kuhifadhi machapisho TLSB

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB), imesema itaendelea kuhifadhi machapisho ya vitabu vya ajili ya kukuza maarifa na elimu kupitia vitabu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya TLSB, Prof. Rwekaza Mukandala, alisema jana Dar es Salaam wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wachapishaji na waandishi wa vitabu.

Mkutano huo wa siku mbili wa wachapishaji na waandishi wa vitabu uliandaliwa na bodi ya huduma za maktaba Tanzania na kufanyika kwenye ofisi za Maktaba Kuu ya Taifa jijini Dar es Salaam.

Alitaja mada mbili zilizojadiliwa kuwa ni utekelezaji wa sheria ya amana kwenye maktaba mtandao jumuishi ya taifa na umuhimu wa ununuzi wa vitabu kwa ajili ya ukuzaji wa soko la ndani.

Prof. Mukandala alisema Sheria ya Amana ya Mwaka 1975 inasisitiza umuhimu wa machapisho yote yanayochapishwa ndani ya nchi kuhifadhiwa kwenye maktaba kuu ya taifa ili kulinda na kuhifadhi urithi wa kitamaduni na kiakili kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Alisema TLSB inatoa jukwaa la kidijitali ambalo linarahisisha uhifadhi, upatikanaji na usambazaji wa machapisho hayo kwa watumiaji wa ndani na nje ya nchi.

"Hii ni fursa kubwa kwa waandishi na wachapishaji wa vitabu katika kuweka hazina ya maarifa na kutambulisha kazi za ndani kimataifa na katika hilo tunapenda kusisitiza ushirikiano wa karibu kati ya TLSB na wadau ili kuhakikisha machapisho yenu yanawafikia wadau wengi," alisema.

Kuhusu ununuzi na matumizi ya vitabu vya ndani, Profesa Mukandala alisema serikali kupitia TLSB imejizatiti kuunga mkono waandishi na wachapishaji wa ndani kwa kununua vitabu vingi vya ndani vyenye maudhui ya kitanzania.

"Katika mwaka huu wa fedha 2025/26 serikali kupitia TLSB imeweka bajeti kubwa katika ununuzi vitabu na machapisho ya ndani hatua ambayo itaongeza hamasa kwa waandishi na wachapishaji wengi wa Tanzania kushiriki katika mchakato wa kukuza maarifa na elimu.

"Nawahimiza washiriki kutumia mkutano huu kama jukwaa la kujadili fursa zinazotokana na utekelezaji wa sheria ya amana na mchakato wa ununuzi wa vitabu itakayotolewa na watoa mada, mawazo yenu ni muhimu kuboresha kazi zetu na kuinua soko la vitabu hapa nchini," alisema.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Salim Msangi, akizungumza wakati wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, walipofanya ziara katika ofisi za mamlaka hiyo, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MOSHI LUSONZO**

# Dakawa, Kibaigwa sasa kung'arishwa kwa taa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MIJI ya kibiashara ya Dakawa wilayani Mvomero na Kibaigwa, Kongwa mkoani Dodoma iliyoko katika Barabara Kuu ya Morogoro- Dodoma, inatarajiwa kuwekwa taa za kisasa za barabarani na kujengwa na maegesho ya kisasa ya malori ili kupunguza ajali na kukuza uchumi kupitia biashara zinazofanyika.

Uamuzi wa kufanya mradi huo mkubwa, umetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kubaini miji hiyo imekuwa sehemu kubwa na kitovu cha biashara kutokana na uzalishaji mkubwa unaofanywa na wakulima wanaozunguka maeneo hayo.

Akikagua barabara hiyo, Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega, aliwataka mameneja Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS ) wa mkoa wa Morogoro na Dodoma kufanyia kazi agizo hilo mara moja.

"Hili ni agizo la Rais Samia ametaka tuhakikishe kwenye barabara kuu zote ikiwamo hii ya Morogoro - Dodoma kufunga taa za barabarani zinazotumia umeme wa jua katika miji inayokuwa ili kuongeza usalama, kupunguza ajali na kuimarisha biashara za wananchi wa maeneo hayo," alisema.

Waziri Ulega alisema mameneja wote wahakikishe miji inang'aa kwa taa za umeme wa jua ambazo ni gharama nafuu na kusisitiza kuwa barabara nzuri ni fursa, hivyo zikiboreshwa zitachochea maendeleo na kukuza biashara haraka.

HABARI KITAIFA

# Kanuni udhibiti usalama majengo zaja

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

BARAZA la Taifa la Ujenzi (NCC) linafanya mapitio ya rasimu ya kanuni za ujenzi na maoni yaliyotolewa na Benki ya Dunia (WB) kuhusu kanuni hizo.

Kazi ya upitiaji wa rasimu ya kanuni hizo inafanywa kwa wiki mbili na timu ya wahandisi chini ya usimamizi wa Mtendaji Mkuu wa NCC, Mhandisi Dk. Matiko Mturi.

Akizungumza wakati wa kikao cha kuitia kanuni hizo, Mhandisi Geofrey Mwakasenga, alisema NCC ina jukumu la kuandaa, kuratibu na kusimamia maendeleo ya viwango, kanuni na miongozo ya sekta ya ujenzi nchini.

"Kanuni hii itakuwa moja ya misingi ya sheria ya ujenzi ambayo pia baraza linasimamia," alisema Mhandisi Mwakasenga.

Kanuni hizo zinatarajiwa kuwa mwongozo wa kitaifa wa kusimamia usalama wa majengo, usalama wa watumiaji, na kuhakikisha majengo yanazingatia utunzaji bora wa mazingira, ndani na nje ya jengo.

Aidha, Mhandisi Mwakasenga alitoa wito kwa wadau wa sekta ya ujenzi kutumia kanuni hizo zitakapokamilika, akibainisha kuwa zitaleta manufaa makubwa kwa kupunguza athari zinazotokana na ujenzi usiozingatia viwango.

"Tunaomba wadau wote wa tasnia ya ujenzi kutumia kanuni hizi mara zitakapokamilika ili kupunguza au kuondoa athari zinazoweza kujitokeza katika ujenzi," alisisitiza.

Naye Msanifu Majengo, Mariahildergard Byarufu, alisema kanuni hizo zitasaidia kuimarisha viwango vya ujenzi na kuhakikisha mazingira rafiki kwa watumiaji wote, wakiwamo wenye mahitaji maalum.

"Kupitia kanuni hizi, majengo yatakuwa na nafasi zinazokidhi viwango vinavyotakiwa, na kuwezesha kundi hili kutumia majengo bila kuhitaji msaada wowote, alisema Arch. Byarufu.

Kwa sasa, NCC inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha kanuni hizo zinakamilika kwa wakati na kuleta mageuzi chanya katika sekta ya ujenzi nchini.



Kaimu Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Abed Gallus (wa tatu kushoto), akitoa maelezo kuhusu maboresho yaliyofanyika katika bandari hiyo, kwa ujumbe kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania (JWT), walipotembelea bandarini hapo juzi, kujionea uwekezaji uliofanyika. Wengine ni Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Hamis Livembe (wa tatu kulia) na (wa pili kushoto) ni Meneja wa Uhusiano wa Kampuni ya DP World Tanzania, Elitunu Mallamia. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## H/shauri Malinyi yazindua Baraza la Wafanyakazi

**Na Joseph Mwendapole**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Malinyi mkoani Morogoro, imezindua Baraza la Wafanyakazi la Wilaya hiyo ili kutoa fursa kwa watumishi kujadili maslahi yao sambamba na kukabili changamoto mbalimbali.

Baraza hilo wajumbe wake wanatoka katika vyama mbalimbali vya watumishi chini ya halmashauri hiyo ikiwa ni pamoja na Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) na Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE).

Uzinduzi wa baraza hilo uliofanyika jana, ulikwenda sambamba na uchaguzi wa Katibu, Naibu Katibu na wajumbe, John John, alichaguliwa kuwa katibu kwa kura 34 huku Neema Mdengero akichaguliwa kuwa katibu msaidizi kwa kura 21.

Akizungumza kwenye kikao hicho, mgeni rasmi, Christina Matage, kutoka Ofisi ya Kazi Mkoa wa Morogoro, alisema halmashauri hiyo inatanua uwanja wa maslahi na utatuzi wa changamoto za watumishi kwa karibu zaidi.

"Baraza hili lina maslahi makubwa kwenu. Litumieni vizuri kuhakikisha changamoto zenu zinatatuliwa. Mkitatua changamoto zenu mtafanya kazi kwa moyo na uadilifu. Katika hili nampongeza sana mkurugenzi (mtendaji wa halmashauri) kuhuisha baraza hili hapa Malinyi," alisema Matage.

Pia aliwapongeza wajumbe waliochaguliwa na kuwaomba kufanya kazi kwa juhudi ikiwa ni kutimiza wajibu wao sambamba na kuweka utaratibu wa kufanya vikao na kujifanyia tathmini mara kwa mara.

Kabla ya uzinduzi wa baraza hilo, ilitanguliwa semina kwa wajumbe kuhusu majukumu mbalimbali ya baraza hilo na malengo yake.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, ambaye ndiye Mwenyekiti wa Baraza hilo, Khamis Katimba, alisema baraza hilo ni moja ya nyezo katika utatuzi wa changamoto mbalimbali kwa pamoja na uimarishaji wa maslahi ya watumishi.

"Kupitia hili baraza tutapanga na kutatua changamoto zetu. Tumefanya hivi ili tuwe tunazungumza kwa pamoja, tunapanga kwa pamoja na tunakubaliana kwa pamoja," alisema.

Pia alisema uzinduzi huo umefanywa wakati mwafaka kwa kuwa halmashauri iko katika hatua ya kupitia Rasimu ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

"Baraza hilo pamoja na kwamba tumelizindua leo, lakini tunapaswa kupitia Rasimu ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 ili tutoe maoni yetu. Ndani ya rasimu ambayo mlishakabidhiwa awali, imezingatia mambo mengi, nililokusudia ni kushirikishana kwa pamoja kwa maslahi ya wananchi na watumishi wote," alisema.

Katibu wa Chama cha Wafanyakazi Wilaya ya Malinyi, Juhudi Swetu, alisema uzinduzi wa baraza hilo unafungua majadiliano ya moja kwa moja kati ya watumishi na ofisi ya mkurugenzi.

Naye Katibu wa CWT Mkoa wa Morogoro, Alphonce Benedict, aliwataka wanachama wa baraza hilo kutumia baraza kueleza na kutetea maslahi yao na siyo nje ya baraza hilo.

Katibu wa TALGWU Mkoa wa Morogoro, Mohammed Mtima alipongeza Rasimu ya Bajeti ya halmashauri hiyo akisema imezingatia stahiki za watumishi.

"Nimepata muda mzuri wa kuisoma, nimeona maslahi ya malipo ya likizo, uhamisho, matibabu, motisha kwa watumishi na bajeti kwa ajili ya vikao vya mabaraza ya wafanyakazi. Imekaa vizuri sana," alisema.

Mwishoni mwa kikao hicho, wajumbe hao kwa pamoja walikubaliana na rasimu ya mapato na matumizi ya halmashauri hiyo 2025/26 kwamba, imezingatia stahiki za wafanyakazi kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni katika utumishi wa umma.

## Songwe yajipanga kwa huduma bora za afya

**Na Moses Ng'wat,** TUNDUMA

WATAALAMU wa sekta ya afya mkoani Songwe wamejipanga kutekeleza mikakati madhubuti kwa lengo la kuhakikisha uendelevu wa usimamizi na utoaji wa huduma bora za afya.

Mikakati hiyo imebainishwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Boniface Kasululu, wakati akiongoza kikao maalum cha uhakiki na tathmini ya ubora wa takwimu za huduma za afya, kilichofanyika juzi katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji Tunduma.

Dk. Kasululu alisisitiza umuhimu wa takwimu katika mfumo wa utoaji huduma za afya nchini.

"Takwimu ni moja ya nguzo kuu za mfumo wa utoaji huduma za afya katika nchi, lakini pia ubora wa takwimu ni msingi wa maamuzi sahihi na ya ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi," alisema Dk. Kasululu.

Aidha, Dk. Kasululu alisisitiza umuhimu wa utoaji wa huduma bora kwa wananchi, akibainisha kuwa serikali imefanya maboresho makubwa katika sekta ya afya.

Alieleza kuwa maboresho hayo ni pamoja na kuleta vifaa tiba, ujenzi wa hospitali, na vituo vya afya pamoja na kuajiri watumishi.

"Miaka mitano iliyopita, Mkoa wa Songwe ulikuwa hauna hospitali ya mkoa na ni halmashauri tatu pekee ndizo zilikuwa na hospitali, lakini sasa hata halmashauri yenu ina hospitali kubwa," alisema.

Hata hivyo, alibainisha kuwa changamoto kubwa iliyosalia ni kuwa na ubora wa huduma zinazotolewa. Dk. Kasululu alisema kwa mwaka huu, mkoa wa Songwe umejipanga kuhakikisha usimamizi wa huduma za afya unaimarishwa zaidi kupitia mshikamano wa viongozi na watumishi wa afya.

Aliwataka waganga wakuu wa wilaya, halmashauri, na menejimenti za hospitali kushirikiana kufanikisha maboresho hayo.

Katika kikao hicho, timu ya wataalamu kutoka ngazi ya mkoa wakiongozwa na Dk. Kasululu itafanya tathmini ya takwimu za huduma za afya za kipindi cha Oktoba hadi Desemba, mwaka jana.

Timu hiyo pia imepanga kutembelea vituo vya afya nane ndani ya siku mbili zijazo na kuandaa mpango kazi wa kuboresha vituo vingine vilivyobaki kabla ya mwisho wa Februari, mwaka huu.



## Magereza sasa kutumia mbolea kiwanda Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza limeingia makubaliano ya kutumia mbolea zinazozalishwa na kiwanda cha Itracom Fertilizer LTD kilichoko jijini hapa, ili kuboresha shughuli za kilimo ikiwamo kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Mkuu wa Jeshi la Magereza nchini, Kamishna Jenerali Jeremiah Katungu, alisema hayo juzi wakati wa maonesho ya ufanisi wa mbolea za FOMI zinazotengenezwa na kiwanda hicho, katika shamba darasa la jeshi hilo lililoko makao makuu, Msalato jijini hapa.

Kamishna Jenerali Katungu aliushukuru uongozi wa kiwanda hicho kwa kuona umuhimu wa kujenga ushirikiano baina yao ambao anaamini utazidi kukuza sekta ya kilimo ndani ya jeshi hilo, ikiwamo kuongeza uzalishaji kutokana na kulima kitaalamu kwa kutumia mbolea stahiki katika mazao ya chakula na biashara.

"Tunawashukuru sana Itracom Fertilizer kwa kukubali kushirikiana nao katika kuendesha shughuli za kilimo naamini tutafika mbali kwenye uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara," alisema Katungu.

Aidha, alisema jeshi hilo litaendeleza ushirikiano na Intracom ili kuzalisha kwa tija ikiwa ni maelekezo ya serikali kuwa Jeshi la Magereza kuongeza uzalishaji ili kujitosheleza kwa chakula.

Kamishna Jenerali Katungu alitoa rai kwa wadau mbalimbali na wananchi kwa ujumla kutembelea shamba darasa la Jeshi la Magereza kwa ajili ya kujifunza mbinu bora za kilimo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alilipongeza Jeshi la Magereza kwa kuingia makubaliano ya ushirikiano na kiwanda hiko ili kuboresha shughuli za kilimo na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara jeshini.

Senyamule alisema kutokana na umahiri lilio nao Jeshi la Magereza kwenye sekta ya kilimo, anaamini ushirikiano wao baina ya kiwanda cha uzalishaji mbolea cha Itracom utazidi kuongeza uzalishaji katika mazao mbalimbali wanayolima.

# Hoja tisa za TUCTA muswada mabadiliko ya sheria za kazi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) limetoa hoja tisa kuhusu marekebisho ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi kwa Mwaka 2024.

Moja ya hoja lilizotoa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, ni likizo ya dharura isiyo na malipo kwa mfanyakazi iwe angalau miaka mitano badala ya siku 30 zilizopendekezwa kwenye muswada.

Aidha, TUCTA imependekeza iwapo mama atajifungua mtoto njiti, apewe muda wa uangalizi wa mtoto mpaka mtoto akamilishe wiki 40 badala ya wiki 36 zilizopendekewa kisha mama apewe likizo ya uzazi ambayo haitaathiri muda wa uangalizi mtoto.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa baada ya kuwasilisha maoni kwa kamati hiyo, Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, alisema lengo la kuongezwa kwa muda wa likizo ya dharura ni kukidhi mahitaji ya mtu ambaye anakuwa kwenye mchakato wa kiuongozi au kimasomo.

Pia alisema muswada unapendekeza kuondoa neno 'Sunday' kwenye tafsiri inayohusu mshahara wa msingi na kwamba wao shirikisho linaona neno hilo libaki kwa sababu ni utamaduni wao wa muda mrefu, hivyo kama kuna haja ya kuongeza neno jipya la 'rest day' basi liongezeke bila kuathiri neno 'Sunday'.

"Muswada pia unapendekeza kuongeza wigo wa tafsiri wa neno 'senior management employee' kwa kujumuisha wafanyakazi wenye mamlaka ya kuajiri, kinidhamu na kusitisha ajira nao kutambulika kama 'senior management employee', TUCTA tumeshauri kamati maana ile ibaki kama ilivyokuwa kwa sababu wafanyakazi wengi watajikuta wanaangukia kwenye kada hiyo na kusababisha kukosa haki zao za msingi ikiwamo malipo ya saa ya ziada na kujumuika kupitia vyama vya wafanyakazi kama ilivyo katika sheria ya sasa," alisema.

Pia alisema TUCTA imependekeza kuwa mfanyakazi anayejiriwa kwa misingi ya kupata mafunzo afanye mafunzo hayo kwa kipindi cha miezi isiyozidi 12 tu kisha aajiriwe kama mfanyakazi kamili badala ya miezi 24 iliyopendekezwa katika muswada.

"Muswada unapendekeza kwenye masuala ya dharura/ majanga mwajiri akae na mfanyakazi kukubaliana namna ya kushughulikia hilo suala. Maoni ya TUCTA ni kuwa pale ambapo kuna chama cha wafanyakazi mwajiri ashauriane na chama hicho ili kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi. Mfano hatima ya ajira na ujira kwa mfanyakazi," alisema.

Rais huyo alisema TUCTA pia inashauri nafuu ya mtu anasitishiwa ajira kwa kutokufuata taratibu au kutokuwapo na sababu zenye mashiko basi alipwe fidia/nafuu ya mshahara kulingana na sheria iliyopo sasa tofauti na mapendekezo ya muswada ambayo yameweka ukomo wa mshahara isiyozidi miezi 12.

"Mapendekezo ya muswada uliopo sasa yatasababisha uwepo wa fidia zisizo na uhalisia na pia kuwapa mamlaka waajiri kusitisha ajira za wafanyakazi pasipo kufuata utaratibu.

"Lakini pia itaondoa maana ya uwepo wa kanuni za utendaji bora tangazo la serikali namba 42 la mwaka 2007 TUCTA inashauri vyombo vyetu vya utatuzi wa migogoro ya kikazi nchini vimekuwa vikifanya kazi yake kwa umahiri mkubwa kwa kutoa fidia zinazostahiki kwa kuzingatia sheria iliyopo sasa," alisema.

Alisema TUCTA pia imependekeza kuwa wakati wa majadiliano ya mkataba wa hali bora za kazi katika taasisi za umma, endapo mkataba utapelekwa kwa Katibu Mkuu kwenye wizara husika, mkataba huo utolewe uamuzi na Katibu Mkuu kwenye wizara husika ndani ya siku 60 badala ya kutokuwa na ukomo wa muda wa kimaamuzi katika muswada wa sasa.

Pamoja na hayo, alisema TUCTA imeendelea kupendekeza kuwa chama cha wafanyakazi chenye mamlaka ya kujadiliana na mwajiri wakati wa kuunda mabaraza ya wafanyakazi kiwe ni kile chama kinachotambulika na mwajiri kama ilivyo kwenye sheria ya sasa na chama kilichosajiliwa na kina wanachama katika eneo hilo.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Alhaji Jabir Shekimweri, akiwasaidia mafundi alipotembelea kukagua maendeleo ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kata ya Matumburu, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC aagiza kukamatwa mali za waliotafuna fedha h/shauri

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ameagiza kukamata mali za watu wanaodaiwa Sh. milioni 36 na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ambazo walizikusanya kama ushuru baada ya kupewa zabuni ya kukusanya mapato lakini hawakuzipeleka benki.

Alitoa agizo hilo jana kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) baada ya Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, kusema watu wanane akiwamo mtumishi mmoja wa serikali wanadaiwa zaidi ya Sh. milioni 37.

Dk. Mganga alisema wananchi saba ambao walipewa zabuni ya kukusanya ushuru wa halmashauri hiyo wanadaiwa Sh. milioni 32.5 wakati mtumishi aliyetajwa kwa jina la Dunstan Simpasa anadaiwa Sh.milioni 5.031.

Alisema mtumishi huyo kutokana na deni analodaiwa na halmashauri aliingia makubaliano na Benki ya NMB awe anakatwa Sh. 100,000 kila mwezi katika mshahara wake.

Alisema wananchi saba walikamatwa na polisi na baadaye wakaachiwa kwa dhamana lakini hakuna muda maalum uliowekwa kwa ajili ya kulipa fedha hizo.

Kutokana na hali hiyo, Dendego aliagiza ifikapo Machi 30, mwaka huu, fedha zote ziwe zimerejeshwa kwa asilimia 100 na ikishindikana, wadaiwa wote vitu vyao vikamatwe.

"Hawa watu wamechukua hela za serikali sasa sioni kama ni sawa kumfanya mtu arudishe hela anavyotaka yeye. Mimi naona si sawa na huyu mtumishi anayerudisha Sh. 100,000 kila mwezi atatumia miaka mitano kurudisha hela aliyoichukua akastarehe nayo lakini sisi tunachelewa kupeleka maendeleo kwa wananchi," alisema.

Dendego alisema katika jambo ambalo hapendi kuliona likijitokeza katika mkoa huu ni watu kuchukua hela za serikali na kuzifuja.



# Makosa 164 dhidi ya binadamu yapunguzwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar kwa mwaka 2024 limefanikiwa kupunguza makosa 164 dhidi ya binadamu sawa na asilimia 12.8 kati ya makosa yote 1,116 yaliyoripotiwa ikilinganishwa na mwaka 2023 ambayo yalikuwa 1,280.

Naibu MKurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Zuberi Chembera, alisema hayo wakati, akitoa tathmini ya hali ya usalama Zanzibar kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2024, Makao Makuu ya Polisi Zanzibar.

Alisema aina ya makosa yaliyoshughulikiwa ambayo yameripotiwa katika vituo vya polisi ni pamoja na mauaji, kubaka na kulawiti.

Alisema kwa Januari 2024 makosa ya kubaka yalikuwa 829 ikilinganishwa na 927 mwaka 2023 sawa na upungufu wa makosa 98.

Aidha, alisema katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2024, jumla ya makosa 217 ya kulawiti yameripotiwa ikilinganishwa na 309 ya kipindi kama hicho mwaka, 2023 upungufu wa makosa 92.

Hata hivyo, alisema makosa dhidi ya binadamu kwa upande wa mauaji yameongezeka na katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2024 jumla ya makosa 66 yameripotiwa ikilinganishwa na 44 ya mwaka 2023, ongezeko la makosa 22 sawa na asilimia 50.

"Makosa mengi ya mauaji yametokana na baadhi ya wananchi kujichukulia sheria mkononi," alisema Chembera.

Kuhusu makosa ya kuwania mali, alisema makosa 1,855 yameripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2024 ikilinganishwa na 1,585 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka 2023 ikiwa ni ongezeko la makosa 270.

Alisema katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2024, jumla ya makosa 823 ya uvunjaji yameripotiwa ikilinganishwa na 833 ya kipindi kama hicho mwaka 2023 ambayo ni upungufu wa makosa 10 sawa na asilimia 1.2.

"Katika kipindi cha Januari - Desemba, 2024, jumla ya makosa 370 ya wizi wa mifugo yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 244 ya kipindi kama hicho mwaka 2023. Hili ni ongezeko la makosa 126 sawa na asilimia 51.6," alisema.

Kuhusu makosa dhidi ya maadili ya jamii, alisema jumla ya matukio 174 ya maadili ya jamii yameripotiwa katika kipindi cha Januari - Desemba, 2024 ikilinganishwa na matukio 176 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka, 2023 ikiwa ni upungufu wa matukio mawili ambayo yalihusisha matumizi ya dawa za kulevya.

Hata hivyo, alisema kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2024, jumla ya matukio 302 dhidi ya watalii yameripotiwa ikilinganishwa na 181 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho cha mwaka 2023, ongezeko la matukio 121.

DCI Chembera, aliwataka Makamanda wa Polisi wa mikoa pamoja na maofisa wa polisi kuongeza nguvu kuzuia makosa ya mauaji, wizi wa pikipiki, wizi wa mifugo, makosa dhidi ya watalii na usalama barabarani ambayo yameongezeka mwaka 2024 ikilinganishwa na mwaka 2023.

Pia, aliwataka kushirikiana na jamii, vikosi vya ulinzi na usalama na taasisi za haki jinai katika utekelezaji wa majukumu yao.



Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (D/DCI), Zuberi Chembera, akizungumza na makamanda wa polisi wa mikoa na maofisa wa jeshi hilo, jijini Zanzibar jana, kuhusu tathmini ya hali ya usalama kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2024. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vifo ajali za barabarani vyaongezeka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATU waliofariki kutokana na ajali za barabarani mwaka 2024 wameongezeka kwa asilimia 23.5 kutoka 189 hadi 153, mwaka 2023.

Mtakwimu Ahdada Hassan Suleiman, kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, alisema hayo wakati akiwasilisha takwimu za ajali na makosa ya barabarani kwa waandishi wa habari visiwani hapa.

Alisema idadi ya ajali za barabarani zilizoripotiwa mwaka 2024 zimeongezeka na kufikia 222 kutoka 193 mwaka 2023.

Alisema kwa mwaka huo wa 2024 Wilaya ya Kaskazini A Unguja, inaongoza kwa kuwa na ajali 38 na kwa mwaka 2023 Wilaya ya Magharib A Unguja iliongoza kwa kuwa na ajali 32.

Aidha, alisema jumla ya waathirika wa ajali 413 wameripotiwa mwaka 2024 na 363 ni wanaume, 50 ni wanawake na Wilaya ya Kaskazini A Unguja imeripotiwa kuwa na waathirika wengi ambao ni 70 sawa na asilimia 16.9 ikilinganishwa na wilaya zingine.

Ahmada alisema waathirika waliojeruhiwa mwaka 2024 wamepungua kwa asilimia 3.4 na kufikia 224 kutoka 232 mwaka 2023.

"Mwaka 2024 miongoni mwa waathirika wa ajali za barabarani waliojeruhiwa na waliofariki, waathirika wengi wameonekana ni abiria ambao ni 164, waendesha baiskeli na pikipiki 142, waenda kwa miguu 91 na madereva walikuwa ni 16," alisema.

Alisema jumla ya ajali 222 zilizoripotiwa mwaka 2024, 163 zimesababishwa na kuendesha gari kwa mwendo wa kasi, 58 zimesababishwa na uzembe wa dereva na moja imesababishwa na hitilafu ya umeme.

Kuhusu makosa ya barabarani, alisema jumla ya makosa 47,258 yameripotiwa kwa mwaka 2024 na 47,161 yameripotiwa kwa wanaume, 97 kwa wanawake.

Alisema kosa kuu lililoripotiwa mwaka 2024 ni kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani yalikuwa 16,487, yakifuatiwa na kuzidisha idadi ya abiria na mizigo 10,070 na kuendesha chombo cha moto bila ya leseni, bima na leseni ya njia makosa 7,901.

Alisema kwa mwaka 2024 tozo zilizolipwa mahakamani kwa kesi 46,933 ni Sh. 1,139,557,301.

## Serikali yajipanga kuimarisha upatikanaji umeme

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema imejipanga kuimarisha huduma za upatikanaji wa umeme vijijini ambazo zitawawezesha wananchi kuacha kutumia kuni na mkaa ambayo ni tishio kwa uharibifu wa mazingira.

Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduwara, alisema hayo wakati akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja katika ziara ya kuzipatia ufumbuzi changamoto za upatikanaji wa umeme na pamoja na kuongeza kampeni za kuacha kutumia kuni na mkaa.

Alisema katika mwaka wa fedha 2024-2025 Wizara ya Maji, Nishati na Madini, imejipanga kuongeza upatikanaji wa huduma za nishati ya umeme hadi vijijini ikiwamo kujenga laini nyingine mpya za umeme.

Alisema serikali imejipanga kuleta megawatti 220 na kuweka waya mpya kutoka Tanzania Bara huko Ras Kilomoni kutokana na waya unaotumika sasa kuwa na uwezo wa megawatti 132 KV.

Alisema umeme huo utakuwa na uwezo mkubwa kwa matumizi ya shughuli nyingi ikiwamo za maendeleo katika miradi ya viwanda na matumizi ya hoteli za kitalii.

Kaduwara alisema kwa upande wa wamiliki wa hoteli za kitalii wamekuwa wakipokea malalamiko makubwa ya kuwapo kwa umeme mdogo usiotosheleza matumizi ya hoteli hizo na kuibuka tatizo la kukatika mara kwa mara.

Aidha, aliwataka wanawake kujipanga zaidi kuingia katika mageuzi yaliopo sasa ya matumizi ya nishati asilia ya gesi na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Alisema hivi sasa maeneo mengi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na Pemba kumejitokeza tatizo la athari za mazingira yanayotokana na wananchi kukata miti kwa matumizi ya kuni na mkaa.



STELLA DAM
UKURASA 14



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# WAELEZE NINI WANAGOMBEA

HAIJAJULIKANA wazi kwa nini msanii kutoka lebo ya WCB, Zuchu na mtangazaji wa Wasafi, Juma Lokole, wamekuwa na ugomvi usiokwisha.

Kila mara mastaa hao wamejikuta wakivutana hasa kutokana na uhusiano wa kimapenzi kati ya Zuchu na kiongozi wa lebo ya WCB, Diamond Platnumz.

Safari hii, Zuchu amekuja na maneno makali zaidi na kumtaka Lokole kumchagulia mwanamke Diamond kama anaona yeye hafai kuwa naye.



Yote yanajiri baada ya Lokole kuhoji kama bosi wake, Diamond Platnumz ana nia ya dhati ya kufunga ndoa na Zuchu.

Hapo ndipo Zuchu alionekana kukasirishwa na kuandika waraka mrefu kwa watangazaji wa Wasafi ambao walikuwa wanajadili redioni kuhusu kama kuna uwezekano wa Diamond kumwoa Zuchu.

"Hebu naomba nitoe tamko, sina haja wala silazimishi mimi kuolewa na Nasibu (Diamond). Ifike hatua mtafute vingine vya kuhoji. [Diamond] hana lazima hata ya kuwa na mimi na sijawahi kumshikia bastola wala kumteka," Zuchu alifoka.


Zuchu aliendelea kutoa nyongo "Maana naona huyo Nasibu akiwa na mwanamke dunia nzima inaacha kazi na kuanza kumwandama. Watu wote, taasisi nzima kipindi na vipindi vyote ikitokea siku hata mtu iwe birthday yake mnatafuta namna mniongelee," alisema.

Hiyo sio mara ya kwanza kwa Zuchu na Lokole kutoleana maneno makali kuhusu uhusiano wake wa kimapenzi na Diamond uliodumu kwa miaka mitatu, jambo ambalo wengi wanajiuliza tatizo gani linalowafanya mastaa hao kutoelewana.

Katika maoni ya watu mbalimbali walitaka Zuchu na Lokole kueleza nini wanachogombea kiasi ambacho visasi vyao vinaishia kwenye vyombo vya habari na kusababisha taharuki kwa wapenzi wao.

BASI SAWA

## Malkia Kareen amtaja mzee Habash



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Malkia Kareen, amesema wazo la kuacha muziki lilizimwa na babu yake ambaye kila siku anajitoa kukilinda kipaji chake.

Akizungumza na EATV, Malkia Kareen ambaye ni mtoto wa aliyekuwa mtangazaji maarufu Gadner G. Habash, amesema alipotoa tamko la kushindwa kuendelea na muziki, alimkalisha chini na kumshauri kuachana na mawazo ya kuacha.

"Aliposikia tamko langu la kuacha, babu alinifuata na kuniambia nisikubali kurudi nyuma, alisema kama familia imefunga na kutoa sadaka kwa ajili yangu kwa nini nikate tamaa," amesema Malkia Kareen.

## Msikieni Steve Nyerere



MWIGIZAJI wa Bongo Muvi, Steve Nyerere, amesema wasanii wengi hawapendi kutangaza maendeleo ya nchi kutokana na kuweka mbele pesa kuliko uzalendo.

Steve Nyerere amesema wakati umefika kwa wasanii maarufu wa Bongo Fleva na Bongo Muvi kuungana katika kutangaza mambo mazuri yanayofanywa na serikali.

"Nawaomba wasanii tusiweke mbele mapato pekee kwa kila kitu, tunahitaji kubadilika kwani tukianza kutangaza nchi kwa maendeleo yanayopatikana tutakuwa tumefanya jambo kubwa," amesema Steve.




## COY MZUNGU AWEWESEKA KUPANDA SGR

MCHEKESHAJI maarufu, Coy Mzungu, amesema amejikuta akipigwa na butwaa na raha aliyopita wakati aliposafiri kwa mara ya kwanza na treni ya umeme.

Coy Mzungu amempongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameweza kutekeleza mradi huo na sasa Watanzania wanajivunia kwa kupata usafiri mzuri na wa haraka.

Msanii huyo alikuwa miongoni mwa wasanii ambao wamesafiri kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma kwa ajili ya kuhudhuria Mkutano Mkuu Maalum wa Chama Cha Mapinduzi.





## Misuli ya Diamond inazidi kuonekana

MWANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, ameingia katika orodha ya wasanii wa Kiafrika waliopiga mkwanja mwingi katika majukwaa ya muziki mtandaoni.

Katoka orodha hiyo inamtaja msanii kutoka Afrika Kuisni, Tyla ndiye anaongoza kwa kupata dola milioni 3.1, sawa na shilingi bilioni 7.8.

Anayeshika nafasi ya pili ni mwanamuziki wa Misri, Mohamed Ramadan ambaye amepata dola 2.8 sawa na Sh. bilioni 7.0 kupitia mtandao wa You Tube.

Diamond anashika nafasi ya tatu kwa kujipatia dola milioni 2.7 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 6.8 kwa mwaka.

## MAGITAA YA DIBLO, DALLY YANAVYOSAHAULIKA

**Na Adam Fungamwango**

MWANZONI mwa miaka ya 1990, kulikuwa na mapinduzi ya muziki nchini Congo DR, ambayo wakati huo bado ilikuwa ikiitwa Zaire.

Muziki wa rhumba na Cavasha ulidorora, ukaja aina fulani ya muziki ya mapigo ya kasi. Yalifanana kiasi na ya Cavasha, lakini yenyewe yaliongezewa vionjo fulani kama, ikiwa pia hata aina ya uimbaji haikuwa ya muda mrefu sana. Waimbaji waliimba kwa dakika kadhaa tu, lakini uimbaji uliokuwa wa kuvutia sana, ila sebene ndiyo ilikuwa inaachiwa inatawala kwa muda mrefu. Wakaupa jina la muziki wa soukous.

Gitaa ongozi, au gitaa la solo, ndilo lililoongoza zaidi muziki huo.  Kwenye magitaa ya solo ndiko kulikokuwa na ushindani zaidi. Na ndiko mashabiki wengi wamuziki Afrika, ikiwamo Tanzania walikuwa wanapenda zaidi.

Karibuni wapiga magita wote hao hawakuwa na bendi rasmi. Walikuwa wakikodishwa na bendi, makundi au wanamuziki mbalimbali waliowahitaji. Hapa nitawataja wapiga solo waliojizolea umaarufu sana hapa nchini kutokana upigaji wao kuwakuna wengi.

**Diblo Dibala**

Huyu ndiye alikuwa kipenzi zaidi cha mashabiki wa muziki Bongo miaka ya 1990 kwenye muziki wa soukous. Upigaji wake kama vile gitaa liko kwenye maji, uliwafurahisha na kuwashangaza wengi. Diblo ambaye ni zao la TP OK Jazz chini ya Franco ambaye miaka ya 1970, alifanya shindano ya kuibua vipaji yeye kushinda. Hakujulikana sana hadi yeye pamoja na marehemu Arlus Mabele walipounda kundi ya Loketo.  Alipiga solo nyimbo kama 'Extra Ball', lakini baadaye alijiengua na kwenda kuunda bendi yake ya Matchatcha. Kwenye bendi ya Empire Bakuba ya Pepe Kalle, aliga solo kwa ufundi wimbo wa 'Pon Moun Paka Bouge'.

**Dally Kimoko**

Ni mpiga solo aliyependwa sana si na mashabiki wa muziki huo Afrika, bali hata na wanamuziki wengi walipenda kufanya naye kazi. Solo lake lilichezeka zaidi na kuwa kwenye mahadhi ya Kiafrika.

Hata mwanamuziki wa Zouk, marehemu Oliver Ngouma alifanya naye kazi.  Karibuni kwenye kila wimbo ambao anaupiga kwenye makundi mbalimbali, mama Soukous Stars, Yondo Sister, Madilu System, Loketo Group na mengine mengi na kote huko, hawakukosa kumtaja kwa kusema 'Dally Kimoko, gitare zanga likwanza'. Maana yake ni kwamba Dally Kimoko, gita lisilokuwa na mikwaruzo.

Amepiga nyimbo nyingi sana ambazo hata hapa hazitoshi kuziandika, lakini kwenye bendi Pepe Kalle alipiga gitaa kwenye wimbo maarufu sana nchini 'Shikamoo Seye', Wabongo wanauita 'Hidaya'. Msikilize pia kwenye 'Inde Monie' ya Kanda Bongoman.

**Benico Ipopolipo**

Naye hakuwa nyuma kwenye upigaji wa solo. Ni mwanamuziki aliyekuwa kwenye bendi ya Zaiko Langalanga, lakini alikuwa akikodiwa kwenye makundi mbalimbali ya muziki nchini Congo DR.

Mkono wake wa gitaa la solo unajieleza kwenye nyimbo za Pepe Kalle kama 'Roger Milla', 'Gerant', na 'Zonga Aime,' ambazo zilipendwa sana na Watanzania. Humpagawisha sana Pepe Kalle mpaka anamwita 'Beniiicooo.' Amepiga solo pia kwenye nyimbo nyingi za Madilu System.

**Nene Tchakou**

Mmoja wa wapigasolo wazuri kabisa nchini Congo DR, waliofanya vema kwenye muziki wa soukous.

Huyu alipiga nyimbo nyingi za Kanda Bongoman, Yondo Sister, Soukous Stars na makundi mengine.

Amepiga nyimbo nyingi, lakini ukitaka kumfaidi sikiliza 'Isambe' ya Kanda Bongoman. Hadi anaitwa 'Tchakutchakutchaku baba ooo ooo'.

**Caen Madoka**

Caen Caen, Caen Madoka, anasikika hayati Aurlus Mabele akimtaja kwenye kibao ya Khadija' na zingine alizopiga akiwa na Loketo Group. Ni miongoni na wapiga gitaa la solo aliyepigia makundi mbalimbali wakati wa soukous na kufanya vema, akijipatia umaarufu na kualikwa huku na kule.

FILAMU

# Shangazi Joy mkombozi

**Na Adam Fungamwango**

Leo tuiangalie filamu iitwayo 'Shangazi Joy' ambayo itakushangaza, kukuhuzunisha, kukufurahisha na kukupa mafunzo kwa wakati mmoja.

Imechezwa na Mahmoud Athumani kama baba, Aisha Nyange aliyecheza kama mama, Ziberi Bakari yeye ni John, Abdulkarim Mwautanga kama Kenedy, Jasmine Mohamed amecheza kama Kendy, na Mwajabu Majema, huyu alicheza kama Shangazi Joy.

Inaanza kwa kuonyesha Shangazi Joy akishuka kwenye bodaboda. Alikuwa ametoka kijijini kwenda jijini Dar es Salaam kwa kaka yake.

Ghafla anavamiwa na vijana wawili ambayo wanampora kitambaa cheusi ambacho walimuona nacho akikifunga fundo kama kuna pesa.

Shangazi huyo ambaye hakuwa mkubwa kiumri ni wastani tu wa miaka 23 mpaka 25 aliamua kuwafukuza, hasa yule mwenye kitambaa mpaka akampata, akamwangusha chini na kukichukua.

Anafika kwa kaka yake na kupokelewa vema pamoja na wifi yake. Hata hivyo wapwa zake, John, Kennedy na Kendy hawakumpokea vema. Alionekana ni mshamba ametoka kijijini, hivyo ni mtu dhalili. Hakumpa kabisa ushirikiano. Walionekana kumyanyapaa na kumpa maneno ya kejeli kiasi cha kumfanya kuwa mpweke. Hata hivyo baba na mama wa watoto hao hawakuipenda hali ile.

Kumbe mmoja wa vijana aliyempora kitambaa cheusi siku ile ni John. Shangazi alimkumbuka alipofika kwa kaka yake, lakini 'akapotezea'. Mwenyewe akadhani amemsahau. John alishajua kuwa ndani ya kitambaa mle hakuna pesa ila ni almasi.

Hivyo akaenda kwanza kwa sonara na kuongea naye kuwa ana mzigo. Akataka kumwibia shangazi yake, lakini ilikuwa ngumu. Siku moja akabambwa na dada yake Kendy chumbani usiku. Alipomuuliza akashindwa kujitetea na kumuunganisha kwenye ile dili. Baadaye akamuunganisha na ndugu yao Kennedy. Hao wote lao sasa likawa moja kuisaka almasi ya shangazi yao wakaiuze ili wagawane pesa.

Wakati huo baba yao anapigiwa simu kudaiwa pesa na benki kutokana na mkopo aliokopa na kuuelekeza kwenye biashara ya miti ambayo haikulipa.

Kwa hiyo nyumba ilitakiwa ipigwe mnada kufikia yote hayo. Kabla yote hayajafanyika, watoto wa mzee huyo bado walikuwa wakihangaikia almasi ya Shangazi Joy ambayo alikuwa akiificha kama mboni ya macho yake.

Ukapikwa wali na kuwekwa madawa ya kulevya ili ale alewe na wampekue mwili mzima wakaweza kuipata, kwani walitafuta chumbani anakolala na Kendy lakini hawakuiona.

Kabla hajala chakula, baba yao anafika. Akamwambia dada yake Joy akapakue kingine. Akala yeye, akalewa na kulala nusu mfu. Alipozinduka kesho yake akauliza, lakini kuna kitu akakigundua.

Wakati huo Joy na kaka yake walikuwa wametoka. Walirudi na gari jipya, kila mtu alishangaa. Gari lilinunuliwa na Joy. Alikuwa ameshaiuza ile almasi ambayo ilikuwa inatafutwa na wapwa zake. Baba aliiweka familia yake chini na kueleza uchafu wote walioufanya watoto wake. Akamwambia mkewe kuwa dada yake huyo ndiye aliyewaokoa kwani asubuhi alimuamsha wakaenda mbali, ndipo alipomweleza ana almasi wakaenda mjini kuuza na kulipa deni lote benki na pesa imebaki nyingi.

Watoto wakabaki na aibu, wakaambiwa wamuombe shangazo yao msamaha.

BT BURUDANI TELE

# Sean Kuti mbona unarudi nyuma?



MWANAMUZIKI na mwanaharakati wa Nigeria Seun Kuti, amefafanua kuwa wengi wanamuona kama mtu hapendi wazungu, lakini ukweli yeye anachochukia ni ukoloni kutoka Ulaya.

Katika chapisho la Instagram, Kuti aliweka wazi kwamba anapinga ukoloni wa Ulaya na ubeberu, lakini hiyo haimaanishi kuwa ninapinga watu wa Ulaya.

Ameeleza kwamba Wazungu wengi wamekuwa washirika katika kupigana na uchoyo na mifumo isiyo ya haki, wakifanya kazi ili dunia kuwa mahali pa haki kwa kila mtu.



## Spyro vumilia yataisha

MWIMBAJI wa Nigeria, Spyro, ameelezea namna anavyokabiliana na changamoto katika tasnia ya muziki kutokana na hali yake inayoamini Ukristo.

Katika mahojiano ya hivi karibuni, msanii huyo alifichua jinsi imani yake ilivyosababisha kukosolewa, kukataliwa na kubaguliwa katika tasnia ya burudani.

“Changamoto yangu kubwa ni ubaguzi kwenye tasnia, unajua nilitoka na chapa yangu ya Jesus boy na nimepata lawama kubwa, nimeburuzwa na ni ngumu kaka, amesema Spyro.


## Cardi B hataki masihara

MAMBO yanazidi kuwa mabaya katika ndoa ya mastaa wa Marekani, Cardi B na mumewe Offset, baada ya wawili hao kuvurugana tena wakati wakiendelea na mchakato wa talaka.

Cardi B alimkabili hadharani Offset, kwa kumtolea maneno makali akimshutumu kwa kuwatelekeza watoto wao na kuisimamisha kesi yao ya talaka.

Akionyesha kufadhaika na tabia ya mume wake, amesema kila mara anamfanyia vituko vinavyomkatisha tamaa jambo ambalo linamkera na kumwona kama mwanaume asiyewajibika.





## Tiwa Savage asema kuna papa watu

MSANII maarufu wa muziki wa Afrobeats, Tiwa Savage, ameibua gumzo baada ya kusema kuna watu wabaya kuliko papa katika tasnia hiyo nchini Nigeria.

Mwimbaji huyo aliweka video katika ukurasa wake wa Instagram, akionekana akiogelea kwa furaha pamoja na papa baharini.

Hata hivyo, baadhi ya mashabiki wake waliotazama video hiyo walitoa maoni mbalimbali, ikiwamo wengine wakimuonya kwamba ni hatari kuogelea na samaki hiyo hatari.

Baada ya maoni hayo Tiwa alijibu kuwa kila mtu alikuwa na wasiwasi kuhusu yeye kuogelea na papa lakini hawajui katika tasnia ya muziki ni hatari zaidi ya papa.

## Stella kawapoteza wengi

MWIGIZAJI kutoka Nigeria Stella Damasus, amefichua kuwa jina lake la mwisho si la ukoo wa asili wa familia yake.

Wakati wa mahojiano ya hivi karibuni, msanii huyo wa filamu alisema jina la Damasus sio la ukoo, bali jina halisi ni Ojukwu ambalo halifahamiki na wengi.

“Kwa miaka mingi, niliitoa ufafanuzi kuhusu jina la Damasus, jina hilo sio la ukoo limetokana na watu kuzoea kuniita na sikujisumbua kulibadilisha,” amesema.





# Mkuu wa wilaya aita wawekezaji

**Na Mary Mosha,** MWANGA

MKUU wa Wilaya ya Mwanga, Mwanahamisi Munkunda, amewataka wawekezaji kuwekeza katika wilaya hiyo kwa kuwa tatizo la maji ambalo lilikuwa kero kwao limeshapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Munkunda alisema hayo jana alipofanya kikao na wadau wa maji na menejimenti ya Mamlaka ya Maji Same Mwanga (SAMWASA) baada ya kutembelea na kujionea mradi wa maji Mwanga/Same/Korogwe ambao awamu ya kwanza imeshakamilika na maji yanatoka katika wilaya za Mwanga na Same.

Alisema awali wawekezaji walikuwa wakishindwa kuwekeza katika wilaya hiyo kutokana na tatizo la maji lakini kwa sasa kupitia serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan. Imekamilisha mradi huo.

"Tunatambua wawekezaji wengi walikuwa wakikataa kuja kuwekeza katika wilaya yetu kutokana na tatizo la maji tulilokuwa nalo lakini serikali imeonesha kwa vitendo kuondoa changamoto zinazowakabili wananchi. Kwa sasa tunapata maji saa 24," alisema Munkunda.

Alisema mradi huo umeliliwa na wananchi kwa muda mrefu lakini Rais Samia amekuja kuumaliza na kutatua kiu ya wana - Mwanga na sasa wanayo maji ya kutosha.

Mkuu huyo alisema lengo la mradi huo ni kuifungua wilaya ya Mwanga kiuchumi na kimaendeleo na kuwataka kuwa walinzi wa mradi huo ili uweze kudumu muda mrefu.

Katika hatua nyingine, Munkunda aliwataka watumishi wa SAMWASA kubadilisha utendaji kazi na kuacha kufanya kazi kwa mazoea ili lengo la serikali na kuwahudumia wananchi wake liweze kutimia.

Mkurugenzi Mtendaji wa SAMWASA, Mhandisi Rashid Mwinjuma, alisema uhitaji wa maji kwa wilaya za Mwanga na Same ni lita za ujazo milioni nane kwa siku huku mradi huo ukiwa na uwezo wa kuzalisha lita za ujazo milioni 55.5 kwa siku, hivyo kuwapo kwa ziada ya kutosha.

Mwinjuma alisema kwa sasa mamlaka hiyo inazidai taasisi za serikali na watu binafsi Sh. milioni 149.23 kwa Mwanga na Sh. milioni 132.22 kwa Same na kuhimiza wananchi kuendelea kulipa ankara pamoja na madeni.

# Mume asimulia mkewe DC Mahawe alivyomuaga kabla hajafariki dunia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MUME wa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, Esther Nahawe, Alexander Samson, amesimulia mke wake alimvyomuaga kabla ya kukata roho,

Samson alisema hayo wakati akitoa taarifa ya maziko ya mkewe huyo aliyefariki dunia Januari 14, mwaka huu, katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Mahawe anatarajiwa kuzikwa keshokutwa nyumbani kwao, Ngaramtoni ya chini, jijini hapa.

Samson alisema mkewe alipata shida ya mapafu baada ya kumalizika uchaguzi wa serikali mitaa Novemba 27, mwaka jana, na Desemba 2, mwaka jana, alikwenda Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dar es Salaam alikokuwa akipatiwa matibabu. Alisema awali aligundulika kuwa na saratani ya titi na alipatiwa matibabu na kupona.

Alisema Desemba 17, mwaka jana, Mahawe alihamishiwa Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo ambako alitibiwa tatizo la mapafu na kupona kisha akaruhusiwa kurudi nyumbani.

"Wakati anaruhusiwa, daktari alitushauri turudi baada ya wiki mbili kwa uangalizi wa kawaida lakini baada ya wiki mbili alipata tatizo la kupumua na Januari 13, mwaka huu, majira ya saa 5:00 asubuhi, tulianza safari kwenda Lugalo kama tulivyokuwa tumeshauriwa na daktari.

"Lakini tulipofika eneo la Kwa Sadala, alisema anajisikia vibaya kwa hiyo angependa aende kwa daktari, tukaamua kumpeleka KCMC akapokewa chumba cha dharura na kupatiwa matibabu," alisema.

Samson alisema ilipofika majira ya saa 7:00 mchana, daktari alisema hawataweza kuendelea na safari ya kwenda Dar es Salaam kwa hiyo ikabidi wakae na kusubiri lakini baadaye safari ilifutwa.

"Ilipofika majira ya saa 7:00 usiku, alihamishiwa chumba cha uangalizi maalum (ICU) lakini hali ilizidi kuwa mbaya na ilipofika majira ya saa 5:00 ya Januari 14, alifariki dunia.

"Lakini kabla ya kukutwa na mauti na hali yake kuwa mbaya, akiwa ICU tulizungumza mambo mengi kisha alitoa barakoa akaniambia ndugu yangu mimi nimefika mwisho angalia watoto," alibainisha.

Kuhusu maandalizi ya maziko yake, alisema: "Marehemu mke wangu Ester tutamzika hapa hapa nyumbani Januari 20, mwaka huu. Nyuma ya nyumba yetu hii kuna eneo lenye migomba, ndipo tutakapoanzisha makaburi ya familia na ibada ya mazishi itafanyika hapa nyumbani."

Mahawe alizaliwa Novemba 5, 1973 katika Kijiji cha Isale, Mbulu mkoani Manyara na ameacha watoto watatu, mmoja wa kike na wawili wa kiume.

Enzi za uhai wake, Mahawe alishika nafasi mbalimbali ikiwamo Ubunge wa Viti Maalum kupitia Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mkoa wa Manyara kati ya mwaka 2015 hadi 2020.

Mwaka 2021, aliteuliwa Mkuu wa Wilaya ya Kigoma na mwaka 2023 alihamishiwa Mkoa wa Songwe na kuendelea na wadhifa huo katika Wilaya ya Mbozi.

Mahawe pia alikuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha wasichana wanapata elimu bora kwa ajili ya maendeleo yao.




Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (MAREMA), Elisha Mnyawi (katikati), akiongoza kikao cha wajumbe wa kamati tendaji cha kujadili namna mbalimbali ya utendaji kazi wao, katika mji mdogo wa Mirerani juzi. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Money Yusuf na Naibu Katibu, Dk. Cutis Msosa. **PICHA: GIFT THADEY**

# DCEA yateketeza shehena dawa za kulevya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) Kanda ya Kaskazini, imeteketeza dawa za kulevya kilogramu 185.35 katika Dampo la Maji ya Chai, Arumeru mkoani hapa.

Pia imeteketeza mirungi kilogramu 154.35 na bangi mbichi kilogramu 31, huku watuhumiwa watano wakikamatwa kwa makosa ya kupatikana na dawa hizo.

Uteketezaji wa dawa hizo ulifanyika jana kwa kuzingatia taratibu zote za kisheria, kwa mujibu wa Innocent Masangula, Mkuu wa Operesheni kutoka DECA Kanda ya Kaskazini.

"Uchomaji wa dawa hizi umezingatia sheria na Mahakama ya Wilaya ya Arumeru iliridhia vielelezo hivyo viteketezwe kwani uwezekano wa kuleta madhara kwa binadamu ni mkubwa endapo zitaendelea kuhifadhiwa," alisema.

Ofisa Sheria wa Mamlaka hiyo, Benson Mwaitenda, akizungumzia baada ya uchomaji vielelezo hivyo, alisema sheria ni kali pale mtu akijihusisha na dawa za kulevya.

Alisema kwa mujibu wa sheria, mtu anaweza kufungwa miaka 30 au maisha jela na chombo chake kilichotumika kusafirisha au nyumba iliyotumika kama ghala la kuhifadhiwa, ikibanikiwa baada ya uchunguzi kuwa walifanya kwa kujua vinataifishwa kuwa mali ya serikali.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii wa DCEA Kanda ya Kaskazini, Saraha Ndaba, alisema mamlaka hiyo inaendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali kama vile wanafunzi, watoto, wanawake na maofisa usafirishaji na Kanda ya Kaskazini inaratibu huduma za matibabu na utengamano kwa waraibu wa dawa za kulevya kwa kushirikiana na asasi za kiraia.

Mmoja wa wananchi walioshuhudia uchomaji dawa hizo, Mary Komba, alipongeza jitihada za serikali kupitia mamlaka hiyo na kuwasihi wananchi wenzake kuachana na matumizi na biashara haramu ya dawa hizo kwa sababu madhara yake ni makubwa kwa taifa na jamii pia.

MAKALA




# Bodaboda inavyoiondosha taxi barabarani bila amri

**Na Adam Fungamwango**

KILA zama na kitabu chake. Mambo yanakwenda yakibadilika. Miaka ya 1970, hadi mwanzoni mwa miaka 2000, usafiri wa haraka ulikuwa ni wa taxi. Mtu akitaka kwenda mahala ambako anadhani usafiri wa umma, Uda au daladala atachelewa, atakachofanya ni kwenda kwenye kituo cha taxi. Usafiri huo utakupeleka popote pale unapokwenda kwa haraka na usalama zaidi kwani utakufikisha pale pale ulipotarajia kufika. Kama ni nyumbani, ofisini, kumbi za starehe, baa, hoteli, hospitali au kwenye ahadi yoyote. Halafu enzi hizo mtu ambaye anakodisha taxi, alionekana ni mwenye uwezo wa kifedha.

Kulikuwa na maeneo maalum ambapo magari hayo yalikuwa yakipaki kusubiri wateja. Vilijulikana kama vitu vya taxi. Vilikuwa maarufu sana kama stendi ya basi zilivyokuwa. Aina ya magari yaliyotumiwa kwa wakati huo, ni Peugeot 404, na baadaye zikaja 504, ambazo watoto wa mjini walikuwa wakiziita 'guruwe'.

Kwa kipindi cha miongo mitatu, kuanzia 1970, 1980, 1990, aina hiyo ya magari ndiyo yaliyotumika sana kwa taxi, lakini baada ya hapo wakati taxi zinaanza karatibu kupungua, kulikuwa na aina tofauti tofauti, lakini Toyota Corolla, ndiyo zilikuwa nyingi zaidi.

Madereva wa taxi kwa wakati huo walikuwa wanajulikana hata kwa majina. Walikuwa ni watu maarufu kwa maeneo wanayoweka vituo vyao.

> Kupanuka kwa miji, hasa sehemu ambazo hazina usafiri wa mabasi au miundombinu ya barabara, kumesababisha bodaboda kuchukua nafasi yake.




Wengi walijulikana kutokana na kazi zao hizo za kusafirisha watu kwa njia hiyo.

Ingawa biashara hiyo bado ipo, lakini imedorora kwa kiasi kikubwa, haipo kama zamani. Kwa sasa dereva taxi ni kazi ambayo kama hutokuwa makini, au hauna watu wako basi utakufa njaa. Biashara hiyo kwa sasa ipo kwenye sehemu muhimu sana kama kwenye mahoteli makubwa, viwanja vya ndege na sehemu zingine zinazofanana na hiyo.

Ukiondoa hapo, sehemu zingine biashara ya taxi imeanza kufa kifo cha asili.

Uwepo na bajaj na bodaboda umeonekana kuondoa kwa kasi biashara ya taxi kwenye ulingo wa biashara.

Zilianza kama utani tu, mwanzoni mwa miaka ya 2000, lakini kwa sasa zimeshamiri kila kona na pembe ya nchi na kuwa usafiri wa kawaida kabisa kwa watu wote.

Tofauti na zamani ambapo anayekodisha taxi anaonekana kibopa, lakini usafiri wa bodaboda na bajaj kwa sasa umekuwa ni sehemu ya maisha ya kawaida kwa watu wote, hao wenye hali ya chini ndiyo kabisa wana uhitaji zaidi.

Kupanuka kwa miji, hasa sehemu ambazo hazina usafiri ya mabasi au miundombinu ya barabara, kumesababisha bodaboda kuchukua nafasi yake.

Mfano jijini Dar es Salaam, mji ulikuwa unaishia Ubungo, lakini kwa sasa maeneo ambayo zamani walikuwa mashamba kama Sinza, Kunduchi, Goba, Boko, Bunju, Gongolamboto kuwa majumba, na ukiteremka kwenye barabara kubwa unaingia ndani tena ambako kunakuwa na usafiri na bajaj na bodaboda tu.

Foleni za magari kwenye miji mikuu pia zimesababisha bajaj, na bodaboda kujichukuliwa 'ujiko', kwani unakuwa ndiyo usafiri wa haraka, kutokana na kutokaa foleni na kuweza kupita sehemu mbalimbali finyu, ambazo mabasi na magari madogo hayawezi.

***Tuma meseji 0716 350534***

## Sierra Lione yamrudisha balozi kwa kashfa ya dawa za kulevya

**FREETOWN,** Sierra Leone

SIERRA Leone imemrejesha nyumbani balozi wake kutoka nchi jirani ya Guinea baada ya gari lake kukutwa na masanduku saba yaliyohifadhi dawa za kulevya aina ya kokeini.

Serikali ya Guinea ilitangaza Jumatatu kulikamata gari la ubalozi wa Sierra Leone na kuwashikilia watu waliokuwa ndani ya gari hilo kwa tuhuma za kumiliki shehena ya dawa hiyo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Sierra Leone, Alhaji Musa Timothy Kabba, alisema kutokana na tukio hilo, serikali imemrudisha nyumbani balozi wake aliyekuwa nchini Guinea, Balozi Alimamy Bangura, ili kutoa maelezo kamili kuhusiana na tukio hilo.

Alisema balozi aliyerudishwa nyumbani hakuwa ndani ya gari hilo na hajakamatwa.

"Balozi hajathibitishwa kuhusika na biashara hiyo," Kabba alisema.

Waziri huyo alisema kiasi cha dola 2,000 za Kimarekani zilipatikana pamoja na masanduku hayo saba. Hata hivyo hakutaja kiwango cha dawa hizo zilizokamatwa.

**BBC**



# Baraza la Mawaziri Israel kuidhinisha makubaliano

**TEL AVIV,** Israel

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amesema Baraza la Mawaziri linatarajiwa kukutana kwa ajili ya kutoa idhini ya mwisho ya makubaliano ya kusitisha vita na kundi la Hamas.

Taarifa kutoka ofisi ya waziri mkuu huyo, ilisema kwamba wanakaribia kutoa idhini hiyo na Baraza la Usalama litakutana kabla ya mkutano wa baraza kamili la mawaziri ili kuidhinisha makubaliano hayo.

Haya yanaelezwa wakati kuna wasiwasi kwamba makubaliano hayo huenda yakacheleweshwa kufuatia madai ya Israel kuwa Hamas wanajaribu kuzuia.

Bado haijulikani kama baraza hilo lingekutana jana au leo, kutokana na hofu ya kuwepo ucheleweshwaji wa usitishwaji wa mapigano katika Ukanda wa Gaza unaotarajiwa kuanza kesho.

Hapo awali, Waziri Mkuu Netanyahu alitishia kuchelewesha kura ya baraza la mawaziri kuidhinisha makubaliano hayo akishutumu Hamas kwa kutaka mabadiliko ya dakika za mwisho kwenye makubaliano hayo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alisema pande zote zilikuwa zinamalizia suala hilo na kwamba ana imani usitishaji mapigano bado utaanza kesho kama ilivyopangwa.

Ingawa timu ya wapatanishi wa Israel walikubali mpango huo baada ya mazungumzo ya miezi kadhaa, hauwezi kutekelezwa hadi uidhinishwe na baraza la mawaziri la usalama na serikali.

Hamas ilisema ilijitolea katika mpango huo, lakini kuna taarifa zilieleza ilikuwa ikijaribu kuongeza baadhi ya wanachama wake kwenye orodha ya wafungwa wa Kipalestina ambao wangeachiliwa chini ya makubaliano hayo.

Ucheleweshaji huo unatokana pia na mashambulio yaliyofanywa na Israel ndani ya Ukanda wa Gaza, baada ya tangazo la kusimamisha vita lililotolewa Jumatano.

Blinken alisema ucheleweshaji kama huo unatarajiwa katika changamoto kama hiyo.

"Haishangazi kwamba katika mchakato na mazungumzo ambayo yamekuwa ya changamoto na yenye hali hii, unaweza kupata mwisho ambao sio mzuri," aliuambia mkutano wa waandishi wa habari akiwa mjini Washington.

**BBC**



Wanajeshi wa DRC wakilinda sehemu ya mji wa Masisi hivi karibuni. **PICHA: ALLIANCE**

# Kagame atema nyongo, asema hatatishwa na yeyote

**KIGALI,** Rwanda

RAIS wa Rwanda, Paul Kagame, ameendelea kulaumu mataifa ya nje kwa kuikosoa nchi yake katika vita vinavyoendelea mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Katika hotuba yake, Rais Kagame, aligusia mambo mengi kuhusu siasa za maziwa makuu, usalama, demokrasia na shutuma zinazoilenga Rwanda.

Vita vya DRC vilichukua nafasi kubwa katika hotuba yake, ikiwamo ripoti ya Umoja wa Mataifa kuitaja Rwanda kulisaidia kundi la M23 linaloendelea kuyachukua maeneo mengi.

Rais Kagame alifafanua kuwa mataifa ya nje yameigeuza dunia kama sehemu isiyo na uthibitisho na ukweli.

"Tunaishi katika ulimwengu ambapo sasa una ushahidi wa kimantiki, vidhibitisho na ukweli wa mambo havipewi umuhimu tena, kinachopewa uzito ni kile ambacho amekisema mtu mwingine hata kama hakina ukweli, tumebebeshwa mzigo mzito katika mzozo huu bila kujali uongo wa lawama zinazotolewa dhidi yetu," alisema Rais Kagame.

Alisema Rwanda inalaumiwa kwa sababu jamii za mashariki mwa DRC zinazotumia lugha ya Kinyarwanda zina mafungamano na nchi yake tangu enzi za ukoloni ilipochorwa mipaka ya mataifa.

Aidha, amelaumu jumuiya ya kimataifa kwa miaka 30 iliyopita kushindwa kuutatua mzozo huo huku ikifahamu mzizi wa tatizo.

"Ni mrejesho gani katika uwekezaji mkubwa kikosi kikubwa kama kile cha umoja wa mataifa nchini DRC? Cha shirika kubwa kama umoja wa mataifa, kikosi chenye kutumia kiasi kikubwa cha pesa, unapata faida gani zaidi ya hali kuendelea kuharibika zaidi, hivi ukiwauliza kwa takribani miongo mitatu MONUSCO imefanya kazi gani watajibu nini? Alihoji kiongozi huyo.



Rais Kagame alisema kwamba lawama za jumuiya ya kimataifa kwa serikali yake haziwezi kusaidia lolote, na akaonya kwamba bila kutatua chanzo cha mzozo huu utaendelea kukua.

"Kama unadhani Rwanda iko mashariki mwa DRC kusababisha matatizo unatakiwa kujiuliza kwa nini imeamua kwenda pale kupigana, pengine hiyo itakusaidia kuelewa baadhi ya vitu ulitakiwa kufanya kutuliza hali ya mambo, lakini kuendelea kutoa ripoti na kutishia haisaidii lolote ngoja niwaeleze tumeteseka vya kutosha katika miaka 30 iliyopita hatuwezi kamwe kukubali kurudi kule tulipotoka haijalishi uwezo na ukubwa wa watesi wetu," alisisitiza.

Aidha, alimshambulia Rais Felix Tshisekedi, kuwa kiongozi mwenye vitisho na anaitawala DRC bila kuchaguliwa kihalali.

"Mtu anayesababisha matatizo katika mzozo huu tunaozungumzia huyu bwana Tshisekedi hajachaguliwa, hata mara moja mihula miwili ya utawala wake hajachaguliwa, na hilo mnalitambua na ndiyo maana awali nimesema siku hizi hakuna kujali ukweli wa kimantiki, kithibitisho kinachotazamwa ni maslahi, hajachaguliwa ninyi mnajua pia, tofauti hamsemi wazi lakini mimi nayasema wazi," alisema Rais Kagame.

**DW**

# MATUKIO KATIKA PICHA



Sehemu ya Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi CCM Taifa (NEC), wakiwa kwenye kikao jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa karavati katika barabara inayoenda eneo la ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Kwamkabara, wilayani Muheza, mkoani Tanga, hivi karibuni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**




Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB), Dk. Mboni Ruzegea, akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano wa siku mbili baina ya TLSB, waandishi na wachapishaji wa vitabu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**




Abiria wa bajaji akiwa amekaa mbele upande wa kulia katika bajaji iliyokuwa barabara ya kuelekea Malamba Mawili Mbezi, Dar es Salaam juzi, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wake. **PICHA: SABATO KASIKA**



Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Purana, Enock Paul (kulia), akimpa mkono wa baraka Mwenyekiti wa Kijiji cha Naepo, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Elias Laizer kwenye tukio la viongozi wa vitongoji na kijiji kumshukuru Mungu kwa kushinda uchaguzi na kuanza kutumikia jamii juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# HADITHI

# Malaika shetani-4

WAKATI mwingine umdhaniavyo binadamu sivyo alivyo. Unaweza kumuona ni mtu mbaya au ana roho mbaya kwa kumuangalia, lakini akawa ni mtu mzuri sana ambavyo hukupata kudhani. Unawezi kukutana na mtu ambaye kwa muonekano na jinsi anavyokutendea ukamuona ni mtu mwema sana. Hata hivyo ndani ya roho yake ana mambo ambayo akikifungulia unaweza kuanguka na kuzirai. Ni mtu mbaya kuliko ubaya wenyewe. Anaficha ukatili na roho yake mbaya kwa kivuli cha kujifanya mwema. Watu hawa ni hatari sana. Kwenye kijiji kimoja kilichopo Bungu, Rufiji kunatokea mauaji ambayo hayajulikani chanzo ni nini. Mauaji hayo yanawahusisha wasichana wawili wanaosoma shule ya sekondari, pamoja na vijana kadhaa. Wananchi wanataka serikali ya kijiji ichukue hatua kwa kuwasaka wauaji ambao wanakitia hofu kijiji cha Mikamba na vya jirani. Je muuaji atapatikana? Ni nani? Fuatilia mkasa huu.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Ni kweli kabisa. Wakati wanachimba shimo ili kufukia maiti, kuna mtu alipita maeneo yale. Ilionekana kabisa kuwa alikuwa ameshaona kitu ambacho si cha kawaida, hivyo alipita kwa kunyata. Hata hivyo aligusa kijiwe ambacho kiliporomoka kutoka juu na kusababisha sauti ya majani ambayo iliwaashiria kuwa kulikuwa na mtu karibu yao. Mtu yule alikuwa anapita au ananyata kuangalia nini wanakifanya.

Walichofanya walikurupuka na kuanza kumkimbiza. Alionekana kuwa na mbio kuliko wao.

Kitu pekee walichofanikiwa kufahamu kutoka kwake, ni kwamba alikuwa kijana mwenye umri wa miaka 23 mpaka 25 hivi. Alivaa fulana nyeusi na jinsi lililochakaa la bluu. Aliwachezesha mdundiko kwenye pori na hatimaye hawakumwona tena. Iliwachukua kama nusu saa kumsaka. Walipochoka kufanya kazi hiyo, walikutana na kuamua kutorejea tena eneo walilofanya mauaji kwa kuhofia kukamatwa. Huwezi kujua aliyewaona anaweza kwenda kuwaambia watu kwenye vijiji wakaja na kuwakuta wanafanya kazi ya kufukia maiti. Huwezi kujua labda wakati wanamfukuza kuna mtu mwingine alipita na kuona maiti na kwenda kuita watu. Ilikuwa ni hatari kuendelea kuifukia. Walichofanya wakatimka kila mmoja. Kazi ya kuua wameshaifanya. Ambacho hakikufanyika ni kuondoa ushahidi. Kuufukia mwili wake. Ungefukiwa haya yote yasingetokea. Kijiji kingekuwa na kazi moja tu ya kumtafuta. Wanakijiji wangeweza hata kutumia mwezi mzima kufanya kazi hiyo asijulikane ameenda wapi. Inawezekana kungeanzishwa hata propaganda kuwa ametoroshwa na mwanaume. Mwanzoni wangeweza kukataa kwa sababu ya tabia yake njema, lakini baadaye kuna watu wangeanza kuunga mkono. Walifanya tukio hilo wangeweza hata kutembeza pesa ili propaganda hiyo ienee na kusadikiwa. Baadaye wazazi wake wangeendelea kumsubiri mtoto wao bila mafanikio. Hiyo ingekuwa salama na wauaji na mtu aliye nyuma ya pazia.

Badala yake wanakijiji wamekuja juu, wanataka kazi ya kusaka wauaji ianze mara moja.

********************************************

Mkutano wa pili wa siri ulifanyika baina ya mtu wa kati na vijana wake watatu haukuwa na muafaka sana. Kilichoamriwa ni kwamba ilikuwa ni lazima atafutwe mtu aliyewaona kwani ni hatari sana kwa usalama wao. Anaweza kutoa siri na vijiji vyote jirani vikaungana kuwasaka na kuwakamata na kuwaua.




**"Sawa tumekuelewa tutafanya kazi hiyo, mwambie mkuu asiwe na wasiwasi." "Chochote kitakachotokea, taarifa itakiwa haraka sana."**

"Kikubwa hata bosi mkuu amejua hili. Amesema pesa nusu iliyobaki hatotoa yote. Badala yake ametoa robo, na robo nyingine itakayobaki ataimalizia pale ambapo atakapopatikana mtu huyo. Anatakiwa apatikane haraka sana kabla ya kusambaza habari hizo."

"Tatizo ni kwamba hatujamwona sura yake, alikuwa nyuma yetu, ila kitu pekee ambacho tunakumbuka alivaa alivaa fulana nyeusi na jinzi la bluu lililochakaa, na kingine nachokumbuka ni kwamba ana nywele nyingi," alisema mmoja wa vijana wa kazi.

"Kama atakuwa mmoja wa wanavijiji vya hapa sawa, lakini kama ametoka vijiji vya mbali, itakuwa ngumu," mwingine alichangia.

"Kama anatoka vijiji vya mbali sisi hatuhusu kwa sababu hatokuwa hatari kwetu. Cha kufanya ni kufanya uchunguzi kujua kama anatoka kwenye vijiji vyetu jirani hapa," mtu wa kati alidakia.

"Sawa tumekuelewa tutafanya kazi hiyo, mwambie mkuu asiwe na wasiwasi." "Chochote kitakachotokea, taarifa itakiwa haraka sana."

***********************************

Anaitwa Feruzi. Ni mkazi ya kijiji cha Bungu. Siku ya tukio alikuwa anatoka kijiji cha jirani kumtazama rafiki yake ambaye ni mgonjwa. Wakati anarejea alikuta tukio la vijana watatu wakimshambulia mtu. Ambacho alichokuwa hakifahamu ni kwamba tayari walikuwa wameshamuua, walikuwa kwenye harakati za kumfukia ili kupoteza ushahidi.

Alijificha kwa sababu alijua akionekana tu, mtu wa pili kuuawa ni yeye. Alianza kujitahidi kupita pembeni huku akinyata asionekane. Hata hivyo jiwe lililoanguka kwenye nyasi kavu liliwashtua waliokuwa wakimshambulia Naima. Mpaka alipokuwa akikimbizwa, hakujua ni nani aliyekuwa akifanyiwa vitendo vile.

Kwa muda wa wiki nzima hali ile ilimtesa sana Feruzi. Ni baadaye ndipo alipogundua kuwa kumbe alikuwa ni Naima. Msichana mrembo kwenye kijiji hicho. Alishika namba moja kwa uzuri. Na hilo lilithibitishwa kwa wanaume kutiririka kumtaka. Kuna awe mpenzi wao na wapo waliotaka kumuoa moja kwa moja. Yeye na wazazi wake hawakutaka kwani walikuwa na ndoto kuwa ya kusoma ili awe daktari.

Siku moja alifuatwa na ndugu yake. Mtoto wa shangazi yake. "Kwani wewe umefanya nini mjomba?" "Kwa vipi?" "Nilipita sehemu nikasikia watu fulani wanasema tumemgundua yule alikuwa ni Feruzi. Kwa hiyo anatakiwa ashughulikiwe. Mimi sikutaka kukaa tena kusikiliza, nikakimbia kukutafuta, lakini sijakuona, leo ndiyo nakuona. Kwa hiyo mjomba kuwa makini kuna watu wanatafuta kukushughulikia." "Du! ahsante sana mjomba Abdu kwa kuniambia hili. Nitakuwa makini kuanzia sasa." "Kwani umefanya kosa gani?" "Ni stori ndefu, ila utaifahamu." Akajibu Feruzi. "Mjomba isiwe ni mmoja wa watu wanaotafutwa na kumuua Naima?" Feruzi alitabasamu. Tabasamu ambalo si halisi, akamjibu "Abdu, wewe bado kijana mdogo sana, dunia hii ina mambo mengi ambayo yanahitaji upembuzi yakinifu ili kuyafahamu. Siwezi hata kuchinja kuku, achilia mbali kuua au kushiriki kumuua binadamu, ila kwenye hii dunia unaweza ukapewa hiyo kesi na ukafungwa." Akajibu. Abdu akamwangalia mjomba wake, akamwonea huruma "Sasa unafanyaje anko?" "Hili lisikusumbue sana, mimi nitajua jinsi gani ya kudili nalo, wewe nenda nyumbani." Feruzi hakutaka kumfafanulia mjomba wake ambaye ana umri wa miaka 15 tu. Mambo yaliyopo ni makubwa kuliko umri wake.

Akichokuwa na uhakika nacho ni kwamba aliyewasikia wakizungumza, ni watu wanaomtafuta kwa ajili ya kutaka kumuua kutokana na kuwaona siku ile alipowafuma wanataka kumfukia Naima baada ya kumuua. Hata yeye alijua hawatolala usingizi wao na waliowatuma mpaka watakapomkamata na kumuua ili kuficha ushahidi. Mpaka sasa hakuwa amemwambia mtu yeyote yule. Kitu alichosaidia baada ya kutoka pale siku ile kwa kukimbizwa ni kwenda tu kuwaambia wanakijiji kuwapo kwa mwili wa mtu. Na wanakijiji walipofika walikuta ni kama kuna watu walikuwa wanataka kuufukia lakini wameshindwa kwa kufumwa au kitu kingine kinachofanana na hicho. Feruzi hakunyanyua mdomo wake kumwambia mtu yeyote kuwa alikuta watu watatu na walimfukuza hadi alipofika karibu na kijiji cha Bungu. Kwa hiyo yeye ndiye binadamu pekee anayejua kuwa Naima ameuawa na watu watatu, ambao aliwafuma wakitaka kumfukia. Ilishindikana kwa sababu waliiacha maiti na kumfukuza. Baada ya kumkosa hawakutaka kurejea tena kwa sababu za kiusalama kwani walijua atakwenda kuwaambia wanakijiji na watafika pale haraka sana na kuwakuta.

**Itaendelea Jumamosi**

## HABARI MICHEZO

# KENGOLD YAPUKUTISHA WACHEZAJI 10

**Na Adam Fungamwangwo**

KLABU ya KenGold imetangaza kuachana na wachezaji 10 ambao iliwatumia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mzunguko wa kwanza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Benson Mkocha, amesema kuachana na wachezaji hao ni ushauri wa benchi la ufundi ambalo lilifanya tathmini baada ya michezo ya mzunguko wa kwanza na kutoa mapendekezo yao.

"Tumeachana na wachezaji 10 na kusajili wengine kwa nia ya kuiokoa timu kutoka ilipo sasa, hatukufanya vizuri na tunaonekana timu kibonde, sasa tunataka kuwa timu tishio kwenye Ligi Kuu.

Matokeo ya mzunguko wa kwanza yametufikisha hapa, kwa sasa tumeamua kupambana na kufanya usajili angalau unaoonyesha mwanga kuwa hatutokuwa wanyonge tena.

"Tumesajili wachezaji wa ndani na nje ya nchi, mchezaji maarufu ni Bernard Morrison na Obrey Chirwa, wengine tumewachukua Ghana na nchi nyingine, kusema kweli tumeridhika na tunaamini tutafanya vizuri mzunguko wa pili wa Ligi Kuu," alisema Mkocha.


Hata hivyo, hakutaka kutaja majina ya wachezaji walioachwa, akisema hatowatendea haki kwa sababu wengi wao wamesajiliwa na klabu zingine, hivyo haitakuwa vizuri kwao na klabu zao mpya.

Ofisa Mtendaji Mkuu huyo pia alikiri kuwa wamemtwaa kocha raia wa Serbia, Vladislav Heric, lakini bado hawajamtangaza rasmi mpaka taratibu zote za vibali zikamilike.

"Ni kweli tumeingia naye makubaliano, lakini kwa sasa hatuwezi kumtangaza mpaka hapo tutakapomaliza taratibu zote za vibali," alisema.

Kocha huyo, aliyekuwa akifundisha, Chippa United na Cape Town za Afrika Kusini, ndiye atakayekuwa Kocha Mkuu kuelekea mzunguko wa pili wa ligi, huku Omari Kapilima akirudishwa kuwa Kocha Msaidizi.

KenGold, inaburuza mkia mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa ligi ikiwa na pointi sita kwa michezo 16 iliyocheza, ikishinda mchezo mmoja, sare tatu na kupoteza michezo 12.




Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja wa Yas, Mwangaza Matotola (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni tano, Husna Ally, aliyeibuka mshindi wa magifti droo ya tisa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasichana michezoni wahimizwa chanjo HPV

**Na Shufaa Lyimo**

WASICHANA wametakiwa kutumia chanjo ya HPV kwa ajili ya kujikinga na saratani ya mlango wa kizazi ili waweze kutimiza malengo yao katika michezo hususani mpira wa miguu.

Hayo yalisemwa jana na Mwakilishi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kwa upande wa wanawake, Meskrem Goshine wakati alipokuwa akitoa elimu kwa wasichana wenye umri chini ya miaka 17 wanaoshiriki mashindano ya 'GIFT' yanayoendelea kwenye uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

"Ninawasihi wasichana muende kupata chanjo ya HPV kwa ajili ya kujikinga na saratani ya mlango wa kizazi ambayo imekuwa ikiua wanawake wengi," alisema Meskrem.

Kwa upande wake Ofisa wa Soka la Wanawake wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Stephanie Kabumba, alisema mafunzo hayo yatawasaidia wasichana kujikinga na saratani hiyo na kuweza kufikia malengo.

"Haya mafunzo yatawasaidia wasichana kujitambua pamoja na kufahamu jinsi gani wajilinde ili waepuke kupata ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi," alisema Stephanie.

Aidha, aliwapongeza wote ambao wameamua kufanikisha mashindano hayo yenye lengo la kuinua vipaji vya soka kwa wanawake.

Kwa upande wake, mchezaji wa timu ya JKT Queens, Yasinta Mitoga, alisema amejifunza mengi kupitia elimu ya ugonjwa huo aliyoipata katika mashindano hayo yanayoendelea na kuahidi kwenda kuyafanyia kazi.

"Nimejifunza mambo mengi ambayo nilikuwa siyafahamu kwa ajili ya kuendeleza malengo yangu ya mpira, nitakwenda kuwa balozi wa kuelimisha wasichana kujikinga na saratani ya mlango wa kizazi, alisema Mitoga.

# JKT Queens yapania ubingwa GIFT

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU za wasichana, JKT Queens imapania kutwaa ubingwa wa michuano mipya ya GIFT iliyoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Timu hiyo leo itacheza mchezo wa fainali wa michuano hiyo na TDS Girls kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha wa JKT Queens, Esther Chabruma alisema wachezaji wake wana morali ya juu kuelekea katika mchezo huo.

"Tunatarajia mchezo mgumu hivyo tunapaswa kuingia kwa tahadhari ili tuweze kupata ubingwa wa mashindano haya, hautakuwa mchezo mwepesi kwa sababu na wapinzani wetu ni wazuri na wamejipanga, lakini lazima tupambane na kufanya kila liwezekanalo tupate ubingwa," alisema Chabruma.

Alisema hawatadharau wapinzani wao kwani lolote linaweza kutokea na kuwataka mashabiki wajitokeze kwa wingi uwanjani kwa lengo la kuwapa hamasa wachezaji.

Wakati huo huo, nyota wa timu hiyo, Mwajabu Mziray, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaibuka na ubingwa wa michuano hiyo ambayo ilianza Januari 7 mwaka huu na kushirikisha timu kutoka nchi mbalimbali za Afrika.

"Mpaka kufika hapa, siri ya mafanikio yetu ni kufanya mazoezi kwa bidii pamoja na kufuata vema maelekezo tunayopewa na benchi letu la ufundi, na hata mchezo huu wa fainali tutafanya hivyo, tutapambana," alisema Mziray.

Aidha, alisema kupitia mashindano hayo wamejifunza mambo mengi ambayo wakiyatumia ipasavyo yatawafikisha mbali.

# TRA yaandaa bonanza la w'biashara

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imeandaa bonanza litakalokutanisha wafanyabiashara wa Kariakoo na wafanyakazi wa mamlaka hiyo kesho ikiwa ni kuelekea kilele cha wiki ya mlipakodi Januari 23.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, alisema lengo la bonanza hilo ni kujenga mahusiano mazuri baina ya pande hizo mbili.

Kwa mujibu wa Mpogolo, bonanza hilo litahusisha michezo mbalimbai ikiwamo ya mpira wa miguu, kukimbia, kuvuta kamba, kukimbiza kuku na michezo mingineyo.

"Bonanza hili pia linafanyika kwa kusema asante kwa kuendelea kulipa kodi na tumepanga kuendelea kulifanya kwa ukubwa zaidi ili pamoja na mambo mengine lisaidie kulinda afya za watu wetu," alisema Mpogolo na kuendelea,

"Bonanza hili litaanza kwa kutembea umbali wa kilomita tano katika eneo la Kariakoo na kuhitimishwa eneo la Kidongo Chekundu ambako ndiko kutakuwapo na michezo mingine," alisema Mpogolo.

Aidha, aliwataka wafayabiashara wote katika eneo hilo la Kariakoo, kushiriki bonanza hilo ili kupata fursa ya kutafakari mambo mbalimbali husus yanayohusiana na shughuli zao.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Kariakoo, Severin Mushi, aliwataka wafanyabiashara hao, kutumia bonanza hilo kama fursa ya kuzungumza na Kamishna Mkuu wa TRA kwa kuwa ni miongoni mwa watakaoshiriki ili kuendelea kupata elimu katika mambo mbalimbali yanayowatatiza kuhusiana na kodi.

"Hiii ni fursa nzuri kwetu wafanyabiashara wa Kariakoo, tushiriki bonanza pamoja na viongozi ambao wanaweza kutupatia majibu au kutuelimisha kwenye baadhi ya mambo yanayotutatiza ni muhimu, tusiiache ipite," alisema Mushi.

Alisema kauli mbiu katika bonanza hilo ni 'Kuzima zote na kuwasha bonanza la TRA' na kwamba wameitumia hiyo ili kuleta hamasa kwa wale wote watakaojitokeza kushiriki.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**UNITED YAICHOMOLEA NAPOLI**

MANCHESTER United imekataa ofa ya pauni milioni 40 kutoka kwa klabu ya Italia ya Napoli kwa ajili ya winga wa Argentina, Alejandro Garnacho mwenye umri wa miaka 20. (*Mirror*)

**WILLIAN ATAKIWA EVERTON**

KLABU ya Everton inafikiria kumnunua mshambuliaji wa zamani wa Chelsea na Brazil, Willian mwenye umri wa miaka 36 ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Olympiakos Desemba mwaka jana. (*Telegraph*)

**CAMBIASO KUIKAMU MAN CITY**

KLABU ya Manchester City italazimika kulipa pauni milioni 67 kumnunua beki wa Juventus na Italia, Andrea Cambiaso mwenye umri wa miaka 24, katika dirisha la uhamisho la Januari. (*Gianluca di Marzio*)

**RASHFORD AWINDWA UJERUMANI**

BORUSSIA Dortmund wameungana na AC Milan kutaka kumsajili mshambuliaji wa Manchester United na England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27. (*Florian Plettenberg, Sky Germany*)

**ZUBIMENDI MAMBO SAFI ARSENAL**

ARSENAL imekubaliana maslahi binafsi na nyongeza kubwa ya mshahara na kiungo wa kati wa Real Sociedad na Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25. (*Football Transfers*)

**ANSU FATI ATAKIWA WEST HAM**

WEST Ham na Tottenham zina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Hispania, Ansu Fati mwenye umri wa miaka 22. (*Sport*)

**REAL MADRID WAMTAKA SALIBA**

REAL Madrid wana nia ya kumsajili mlinzi wa kati wa Arsenal na Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 23, msimu wa majira ya joto. (*Foot Mercato*)

**AL HILAL YAKOMAA NA SALAH**

KLABU ya Al-Hilal ya Saudi Arabia imeanzisha tena mazungumzo na wawakilishi wa mshambuliaji wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 32 kwa nia ya kumsajili. (*L'Equipe*)

**AWONIYI KUTUA WEST HAM**

WEST Ham inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Nottingham Forest na Nigeria, Taiwo Awoniyi mwenye umri wa miaka 27. (*Florian Plettenberg*)

**WISSA AIVUTIA NOTTIGHAM**

NOTTINGHAM Forest inamfuatilia kwa nia ya kumsajili mshambuliaji wa Brentford na DR Congo, Yoane Wissa mwezi huu. (*Telegraph*)

**SCHADE NJIANI KUTUA DORTMUND**

KLABU ya Borussia Dortmund inavutiwa na winga wa Brentford na Ujerumani, Kevin Schade mwenye umri wa miaka 23. (*Bild*)

**ATALANTA YAKOMAA NA EDOUARD**

KLABU ya Atlanta United imetoa ofa ya pauni milioni 15 kwa mshambuliaji wa Crystal Palace, Odsonne Edouard, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Leicester City. (*Mail*)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK: LIVERPOOL IPO KWENYE UBORA

**LIVERPOOL,** England

**Nahodha huyo amesema matokeo waliyoyapata mechi za nyuma yanatokana na ubora wa...**

VIRGIL van Dijk amecheka kuhusu madai kwamba Liverpool kwa sasa ipo kwenye kiwango duni.

Majogoo hao walifurahia mwanzo mzuri wa maisha chini ya kocha mpya Arne Slot lakini wamevumilia kushuka kwa kiwango cha juu katika wiki za hivi karibuni.

**Wameshinda mechi tatu pekee kati ya saba zilizopita za Ligi Kuu England na kuruhusu Arsenal kuwakaribia na sasa wamapishana pointi nne kwenye kilele cha msimamo wa ligi.**

Liverpool pia ililala 1-0 dhidi ya Tottenham Hotspur katika mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Kombe la Carabao, lakini Van Dijk alisema matokeo ya hivi karibuni ya timu hiyo ni ushahidi wa kiwango cha juu cha ushindani katika Ligi Kuu ya England.

"Ooh, kwa hiyo tuko kwenye mgogoro sasa?" Alisema Van Dijk kwa kejeli alipoulizwa kuhusu kiwango cha sasa cha Liverpool.

"Inathibitisha tu kwamba Ligi Kuu ya England ngumu sana ambapo unacheza dhidi ya wapinzani ambao ni wazuri sana. Ilikuwa ngumu kila wakati, sawa na Manchester United wakiwa nyumbani na kocha wao mpya na mpango wa mchezo ambao wamekuwa wakionesha.

“Kila mchezo ni mgumu, lazima tutafute njia ya kushinda na nadhani kama tutacheza kama tulivyocheza kipindi cha pili na kuendelea kupambana, tuendelee kujaribu, tuendelee kutafuta nafasi basi nina imani kubwa tutafunga mabao."

Van Dijk pia alitoa maoni chanya katika mwenendo wa hivi majuzi wa Liverpool wa kuruhusu bao la kwanza katika mchezo mmoja. Wekundu hao wamelazimika kutoka nyuma mara tano katika mechi zao saba zilizopita.

"Inaonyesha ujasiri," Van Dijk alisisitiza. "Hakuna anayetaka kutoka nyuma, tunapaswa kuendelea kufanyia kazi hilo na kuwa na kila mtu katika hali nzuri zaidi kuzuia hilo.

Tunachoweza kufanya ni kujaribu kufanyia hivyo katika mchezo unaofuata," alisema.



# NEYMAR: MBAPPÉ ALIMWONEA WIVU LEONEL MESSI

**SAO PAULO,** Brazil

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Neymar, amesema mchezaji mwenzake wa zamani wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappé alipata 'wivu kidogo' baada ya Lionel Messi kujiunga na klabu hiyo ya Ufaransa Agosti 2021 kwa uhamisho wa bure.

Akizungumza katika mahojiano na podikasti iliyoandaliwa na mshindi wa Kombe la Dunia na Brazil, Romário iliyotolewa Alhamisi, Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 32, ambaye amekumbwa na majeraha katika klabu ya Al Hilal ya Saudi, alisema kuwa vivu huo uliathiri uchezaji wa PSG katika mechi kubwa.

Neymar alitoa maoni yake baada ya Romário kumuuliza kama Mbappé, ambaye alijiunga na Real Madrid msimu huu kama 'inamuuma'

"Hapana, sio. Nina vitu vyangu naye, tulipigana kidogo, lakini alikuwa mchezaji wa msingi kwetu alipofika. Nilikuwa nikimwita golden boy," alisema Neymar.

"Siku zote nilicheza naye, alisema atakuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi. Siku zote nilisaidia, nilizungumza naye, alikuja kwangu, tulikuwa na chakula cha jioni pamoja.

"Tulikuwa na miaka mizuri ya ushirikiano, lakini baada ya Messi kuja alikuwa na wivu kidogo.

Akataka kunitenganisha naye. Kulikuwa na mabadiliko ya tabia."

Mbappé alijiunga na PSG kutoka Monaco mwaka 2017, mwaka huo huo Neymar alihama kutoka Barcelona hadi klabu hiyo ya Ufaransa katika moja ya uhamisho mkubwa katika historia ya soka.

Wote wawili walisajiliwa huku klabu hiyo ikitafuta taji lake la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambalo bado haijashinda.

Neymar alisema timu hiyo mara nyingi ilitatizika kutokana na ubinafsi mkubwa, lakini hakumtaja mtu yeyote.

"Ni vizuri kuwa na ubinafsi, lakini lazima ujue kuwa hauchezi peke yako," alisema Neymar.

"Kuna haja ya kuwa na mtu mwingine kando yako. Ubinafsi mkubwa ulikuwa karibu kila mahali, hauwezi kufanya kazi. Ikiwa hakuna anayekimbia na hakuna anayesaidia, haiwezekani kushinda chochote."

# Amorim akunwa na 'Hat trick' ya Amad

**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim amesema anashukuru kwamba 'hat trick' ya Amad ya dakika za lala salama dhidi ya Southampton 'ilisaidia' mazungumzo ya baada ya mechi na mmiliki mwenza wa Manchester United, Sir Jim Ratcliffe kwenda vizuri.

United ilikuwa ikikabiliwa na kushindwa na klabu iliyo mkiani mwa msimamo wa Ligi Kuu England kabla ya Amad kufunga mara tatu ndani ya dakika 12 na kupata ushindi mnono wa mabao 3-1.



Amorim alizungumza na Ratcliffe baada ya mchezo huo na kusema anashukuru kwa mabao ya raia huyo wa Ivory Coast kabla ya kukutana na bosi wake.

"Nilikuwa na dakika tano na Ratcliffe kuzungumza kuhusu mambo tofauti," alisema Amorim.

"Haukuwa mchezo mzuri, lakini matokeo yalisaidia mazungumzo! Tunaendelea kufanya kazi yetu, leo (juzi) ilikuwa muhimu zaidi kushinda, najua mashabiki wanataka kuona soka bora zaidi, lakini tunahitaji kushinda michezo. Tumefanikiwa kushinda na tunaenda kujiandaa kwa mchezo ujao."

United ilikuwa na wakati mgumu muda mwingi wa mchezo dhidi ya Southampton na walikuwa nyuma kwa 1-0 hadi mapumziko.

Amad, ambaye alitia saini mkataba mpya wa miaka mitano wiki iliyopita, alifunga bao la kusawazisha dakika ya 81 na kumalizia hat trick yake ya kwanza katika dakika ya nne za mwisho.

"Labda moja ya wiki bora zaidi maishani mwangu," alisema. "Nimefurahi sana kwa ushindi huu. Timu hii ilistahili kushinda mchezo huu hivyo nina furaha sana.

"Tunajua tuna wachezaji wenye ubora katika timu hii. Tunahitaji wakati mwingine kuwa na njaa zaidi katika nafasi ya tatu ya mwisho.

"Leo (juzi) tulionesha mwishowe tulikuwa timu bora. Nina furaha sana kwa ushindi wa leo kwa sababu timu hii inastahili."

Amad amekuwa mchezaji muhimu zaidi wa Amorim kwa haraka na kocha huyo mkuu wa United alimwambia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 atahitajika tena Brighton watakapozuru Old Trafford kesho Jumapili.

"Anapaswa kupumzika, kula chakula kizuri na Jumapili tunamuhitaji tena," alisema Amorim.

# Endrick ampa mabao yake Antonio Rüdiger

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Endrick alimsifu mchezaji mwenzake Antonio Rüdiger kwa kumwongoza katika ukame wake wa mabao, akitoa mabao yake mawili katika ushindi wa 5-2 wa Copa del Rey dhidi ya Celta Vigo siku ya Alhamisi kwa beki huyo.

Madrid walinusurika na hofu katika mechi ya 16 bora kwenye Uwanja wa Santiago Bernabéu, Celta walipokuwa mbele kwa mabao 2-0 hadi kusawazisha katika dakika ya 91, kabla ya wenyeji kufunga mabao matatu, mawili kutoka kwa Mbrazil huyo katika muda wa ziada.

Endrick mwenye umri wa miaka 18, alianza msimu vyema, akifungua akaunti yake katika LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini hakufunga tangu Septemba 17 na amecheza jumla ya dakika 83 tu za ligi msimu huu.

"Ninaendelea kufanya kazi kila siku," alisema Endrick akiiambia Real Madrid TV.

"Mabao yangu mawili ni kwa Antonio Rüdiger. Anajua anachonifanyia kila siku. Hajawahi kunisifu, na hilo ni jambo zuri. Ananiambia nini cha kufanya, kufunga, kukimbia, kuendelea kupambana. Jana (juzi) kwenye mazoezi alinipa mchezo mgumu nilikuwa nikifikiria nikiwa nyumbani na yeye ni mtu mzuri.

Bao la kwanza la Endrick liliwekwa wavuni kutoka kwenye ukingo wa eneo la hatari ambalo kijana alishangilia kwa kuvua jezi yake huku pili likiwa ni kisigino chenye kufikiria haraka ndani ya kisanduku cha yadi sita.

"La kwanza lilikuwa bao muhimu sana kwangu," alisema Endrick alipoulizwa kuhusu kushangilia kwake kwa furaha na kuvua jezi yake.

"Hii ni kazi yangu, lazima nifanye vizuri kwa timu, kufunga mabao, kufanya chochote, kufunga goli kwa Madrid.

"Katika mchezo uliopita wa Copa nilikosa nafasi, lakini leo (juzi) nimepata nafasi."

# Yanga ni gusa, achia twende robo fainali

INATOKA UKURASA 24

kwa kila timu kusaka nafasi ya kuingia robo fainali. "Kampeni yetu ilianza hatua za awali na kufanikiwa kupata matokeo mazuri katika michezo yetu tuliyoicheza hivyo tunaamini kesho (leo) tutapata matokeo mazuri," alisema Benyahya.

Kwa upande wake, mchezaji MC Alger, Zakaria Draoui alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa pande zote.

"Sisi tunafahamu umuhimu wa mechi hii, lazima tucheze kwa maamuzi ambayo yatatusaidia kuingia hatua inayofuata," alisema Draoui.

# Mashabiki Simba kuangalia mechi Mwembeyanga

INATOKA UKURASA 24

hangilia kelele zao ziwafikie wachezaji na kuwatia moyo, lakini hiyo yote hairuhusiwi na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).

"Awali kulikuwa na maoni mengi kuwa tuweke televisheni kubwa Uwanja wa Uhuru, ili kelele za mashabiki zikipigwa ziweze kuwafikia wachezaji, ukweli ni kwamba hairuhusiwi mita 1,000 kutoka uwanja wa mechi kuwa na shughuli za kimichezo katika eneo hilo, kwa hiyo mawazo na maoni hayo hayawezekani na tukifanya hivyo tunaweza kuadhibiwa tena.

Wengine walishauri mashabiki wasimame barabarani hadi uwanjani ili wachezaji wakipita wapigiwe makofi, hiyo nayo hairuhusiwi, tunawaomba wanachama na mashabiki wa Simba wakae mbali na Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili, kwa sababu macho ya waangalizi yatakuwa hapo, mechi ikiisha, kuanzia robo fainali mfumo wa maisha yetu utaendelea kama kawaida," alitahadharisha.

CAF, iliifungia Simba kuingiza mashabiki kwenye mchezo huo, baada ya vurugu zilizotokea Desemba 15 mwaka jana kati ya timu hiyo dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia ambapo ilishinda mabao 2-1.

Katika mchezo huo, mashabiki wa Simba na CS Sfaxien, walipigana na kusababisha viti kadhaa kung'olewa.

Akiuzungumzia mchezo huo, alisema ni muhimu kwao kwa sababu wanahitaji kuongoza kundi A japo wameshatinga robo fainali.

Wakati huo huo, klabu hiyo imesema tayari jumla ya Shilingi milioni 47 zimechangwa na mashabiki wa timu hiyo katika kampeni ya 'tunawajibika pamoja' kwa ajili ya kulipia fainali ya dola 40,000 walizotozwa na CAF.

"Pesa zilizopatikana mpaka sasa ni Shilingi milioni 47, 141, 024, na iliyobaki ni Sh. milioni 52, 858, 976," alisema Ahmed.

Ahmed alisema iwapo haitotimia klabu itaongezea kilichobaki na kama kiasi kitazidi basi kitatumika kwa matumizi mengine ya timu.

# WACHEZAJI TABORA UNITED WABADILISHIWA MAZOEZI

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Tabora United, Anicet Kiazayidi, ameamua kubadilisha ghafla 'programu' ya mazoezi kwa wachezaji wake baada ya kusikia Ligi Kuu Tanzania Bara itarejea tena wiki ya kwanza mwezi Februari badala ya Machi Mosi.

Awali, kikosi hicho ambacho kilikuwa kimerejea kambini, kilikuwa na aina nyingine ya mazoezi, lakini Bodi ya Ligi ilipotangaza kuwa Ligi Kuu itarejea mapema zaidi kuliko mwanzo, kocha huyo ameamua kuzidisha dozi kwa wachezaji wake.

Hilo limebainishwa na Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Khalfan Mbonde, ambaye alisema walianza mazoezi taratibu kwa lengo la kuongeza kasi kadri muda unavyokwenda, lakini baada ya taarifa ya Bodi ya Ligi, kila kitu kimebadilika.

"Tulianza mazoezi, lakini kwa sababu tulijua ligi itarejea mwezi Machi, tulikuwa na aina nyingine ya 'programu', twende kidogo kidogo na kuongeza kasi taratibu kadri muda unavyozidi kwenda juu.

Lakini baada ya kusikia ligi inarejea mapema, 'programu' imebadilika, tumeongeza kasi na dozi kubwa kwa wachezaji ili kuendana na muda, tunaamini mzunguko wa pili tutafanya vizuri zaidi kuliko hata wa kwanza. Mzunguko wa kwanza tulifanya vizuri, lakini kuna vitu tuliona vimepungua, tumekuja kuviongeza kwa ajili ya mzunguko wa pili," alisema kocha huyo.

Kuhusu usajili, alisema tayari wameongeza wachezaji sita kipindi cha dirisha dogo la usajili hivyo kuwataka mashabiki wa timu hiyo wasiwe na wasiwasi kwani kikosi kitakuwa bora zaidi kuliko kulivyokuwa mzunguko wa kwanza.

"Tumesajili wachezaji sita, mashabiki wa Tabora United wasiwe na wasiwasi, lengo letu ni lile lile, tukikosa ubingwa na nafasi ya pili, basi tusikose ya tatu au ya nne, yaani msimu ujao tunataka kucheza michuano ya kimataifa," alisema Mbonde.

Baadhi ya wachezaji iliyowasajili ni kiungo mkabaji, Cedric Martial Zemba, raia wa Cameroon aliyekuwa akichezea klabu ya Touranga ya Morocco, na kipa Jean Noel Amonome, raia wa Gabon, aliyekuwa akiichezea Arta Solra7 ya Djibouti.



Kocha wa Yanga, Saed Ramovic (kushoto) na nahodha wa timu hiyo, Dickson Job, wakizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) jana kuhusu maandalizi yao kuelekea mchezo wa leo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya MC Alger ya Algeria utakaochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

# KMC yaongeza watano dirisha dogo

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya KMC, imefunga dirisha dogo la usajili kwa kuwaongeza wachezaji watano ambao imesema watakiongezea nguvu kikosi kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Khalid Chukuchuku, amesema jana kuwa wachezaji hao wamesajiliwa baada ya benchi la ufundi na viongozi kuona kuna umuhimu wa kufanya hivyo hasa baada ya matokeo ya mzunguko wa kwanza.

Chukuchuku, amewataja wachezaji wawili tu kati ya hao, ambao ni Hamad Pipino, akisajiliwa kutoka timu ya vijana chini ya miaka 20, Ngorongoro Heroes na Deusdedith Okoyo akitokea Polisi Tanzania.

Mbali na kuichezea Polisi Tanzania, mchezaji huyo pia amewahi kuzichezea klabu za Geita Gold na JKT Tanzania.

Ingawa hakutaja wengine, lakini mmoja wapo ni straika wa zamani wa Simba na Azam, Shaaban Chilunda.

"Benchi la ufundi na viongozi waliona kuna umuhimu wa kukiongezea nguvu kikosi, hasa kutokana na matokeo tuliyoyapata kwenye mzunguko wa kwanza hivyo tukalazimika kwenda sokoni kutafuta baadhi ya wachezaji kwa ajili ya kutuongezea nguvu, leo nitawataja wawili ambao ni Pipino aliyetokea timu ya Ngorongoro Heroes ambapo amekuwa na mchango mkubwa, tukaona bora tumsajili, mwingine ni Okoyo akitokea Polisi Tanzania," alisema Ofisa Habari huyo.

Mbali na hao, alisema wachezaji wengine watawaweka kwenye kurasa zao za mitandao ya kijamii wakati wowote kuanzia sasa.

"Ukiacha hao, kuna straika mkubwa tu ambaye tutamtangaza wakati wowote kuanzia sasa, tunakamilisha vitu vichache, ameshawahi kuichezea Azam FC, Simba na amecheza ligi nje ya nchi," alisema Chukuchuku, akimaanisha Chilunda.

"Tumewasajili wachezaji wa Kitanzania waliokuwa wanacheza Ligi Kuu nchini Malawi kwa ujumla tumefanya usajili wa wachezaji watano, mashabiki wengi hawawafahamu lakini ni wachezaji wazuri watu watawaona muda utakapofika," alisema.

# Michezo

Jumamosi Januari 18, 2025

Nipashe




Amorim akunwa na 'Hat trick' ya Amad UKURASA 22



Winga wa Manchester United, Amad Diallo (mwenye jezi nyekundu), akipiga mpira kufunga goli kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Southampton juzi usiku, United ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAOP**

# *Yanga ni gusa, achia twende robo fainali*

●●● Kikosi hicho leo kina kazi moja tu mbele ya Waarabu, kuhakikisha kinapata ushindi utakaowapeleka hatua hiyo kwa...

**Na Shufaa Lyimo**

HATIMA ya Yanga kufuzu hatua ya robo fainali itajulikana leo baada ya mchezo wao wa mwisho hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya MC Alger ya Algeria utakaochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Yanga inayotamba na msemo wao wa hamasa wa 'gusa, achia twende kwao' leo watakuwa na kazi moja tu ya kugusa kuachia kwenda robo fainali, ikimaanisha ushindi wowote watakaoupata utawavusha kutinga katika hatua hiyo kwa mara ya pili mfululizo.**

Kabla ya mchezo wa leo, Yanga imepishana kwa pointi moja na wapinzani wao wenye pointi nane na kushika nafasi ya pili kwenye kundi huku Yanga wakiwa na pointi saba wakishika nafasi ya tatu.

Hii inamaanisha kama Yanga watakubali kipigo au sare yoyote itawapa nafasi MC Alger kuungana na Al Hilal kutinga hatua hiyo huku Yanga na TP Mazembe zikiaga michuano hiyo.

Kuelekea katika mchezo huo wa leo, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, alisema wamejipanga kupata pointi tatu katika mchezo huo ili wafuzu hatua inayofuata.

Alisema kuwa wanatambua mchezo huo ni muhimu kwao, hivyo amewataka mashabiki wajitokeze kwa wingi kuiunga mkono timu yao waweze kufuzu hatua ya robo fainali.



"Kila siku malengo yetu ni kushinda, tumejiandaa vizuri na kila mchezaji na morali ya juu kuhakikisha tunakwenda kutimiza malengo yao," alisema Ramaovic.

Alisema anafahamu mchezo utakuwa mgumu kutokana na aina na wapinzani wanaokutana nao, lakini wana faida ya kucheza mbele ya mashabiki wao ambao anaamini watajitokeza kwa wingi uwanjani.

"Tutacheza kwa nidhamu kubwa sana, tuna mbinu zetu tutakazozitumia ambazo naamini zitatupa ushindi, hatutawapa nafasi ya kuutawala mchezo, kwa sababu hiyo itakuwa tatizo kwetu," alisema Ramovic.

Kwa upande wake, Nahodha wa Yanga, Dickson Job alisema wao kama wachezaji wapo tayari kwa mchezo wa kesho (leo) na kusema wanahitaji matokeo mazuri ili wafanikiwe kuingia hatua ya robo fainali.

"Tunaelewa umuhimu wa mchezo wa kesho (leo), tunatambua ukifanya kosa moja itakuwa tatizo kubwa, kumaliza mechi nyumbani ni faida kwa sababu tunakuwa karibu na mashabiki wetu, tutapambana kuhakikisha tunashinda mchezo huu kwa sababu kinyume cha hapo tunaondolewa kwenye mashindano, mashabiki waje watuunge mkono na kutupa sapoti yao," alisema Job.

Aidha, Kocha Mkuu wa MC Alger, Khaled Benyahya, alisema mchezo huo ni muhimu na hivyo wamejipanga kukabiliana na Yanga licha ya kuwa ugenini.

Alisema japokuwa Jiji la Dar es Salaam lina joto kuliko Algeria hana wasiwasi kwani wapo tayari kucheza kwenye mazingira yoyote.

Alisema kuwa mchezo huo utakuwa mgumu kiufundi kutokana na umuhimu

INAENDELEA UK. 23

# Mashabiki Simba kuangalia mechi yao M/yanga

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya klabu ya Simba kufungiwa kuingiza mashabiki kwenye mchezo wao wa leo Uwanja wa Benjamin Mkapa, uongozi wa klabu hiyo umepanga kuwapeleka mashabiki katika viwanja vya Mwembeyanga kwa ajili ya kuangalia mchezo huo wa Kundi A.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema baada ya maoni mengi kutoka kwa watu mbalimbali, Simba na wadhamini wao wameamua kwenda kufunga televisheni kubwa kwenye viwanja hivyo vilivyoko maeneo ya Temeke jijini Dar es Salaam ili kuwapa nafasi wanachama na mashabiki waliokuwa wanataka kwenda kuangalia mchezo huo Uwanja wa Benjamin Mkapa, kwenda kwenye viwanja hivyo kwa ajili ya kuishuhudia timu yao.

"Kwa kuwa watu wana maumivu makubwa, na wanachama na mashabiki wa Simba wamezoea kukaa pamoja kijamaa kwa ajili ya kuangalia mpira, sisi na wadhamini wetu tumetenga eneo maalum ambalo wanachama na mashabiki wa Simba watakwenda kuangalia mechi hiyo dhidi ya CS Constantine, eneo tulilolipanga ni Temeke Mwembeyanga.

Tutakuwapo kuanzia saa 5:00 asubuhi, tutakuwa na TV kubwa sana, tutakuwa na burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali," alisema Ahmed.

Alisema awali kulikuwa na mapendekezo kuwa ifungwe TV kubwa, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam ili mashabiki wakutane hapo na watakapokuwa wanas-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >